Nipashe
Jumanne Oktoba 31, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
ISSN 0856 • Na. 0581480
MWANGA WA JAMII
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

UKURASA WA 4
Kinana ashangaa baadhi viongozi kutoheshimika





UKURASA WA 4
Rais Mwinyi asisitiza uadilifu vikosi vya ulinzi

## UDANGANYIFU KWENYE NDOA

# Maombi upimaji DNA yaongezeka

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko pamoja viongozi na watumishi wa Bunge baada ya kumpokea Dk. Tulia jana katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma, alipowasili nchini baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) hivi karibuni jijini Luanda, Angola. **PICHA:BUNGE. Habari Uk. 4**

## Ripoti ya CAG, Bima ya Afya kutikisa Bunge

UKURASA 3



## Majaliwa ataka kasi ya udhibiti magendo katika viwanja vya ndege

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAMTAJA ROBERTINHO DABI UK.24 KATUNI UK.6



Wauzaji wa miwa katika Soko la Tandale Dar es Salaam, wakiiweka kando ya barabara kusubiri wateja juzi, baada ya kukosa eneo la kufanyia biashara kutokana na soko lao kuwa kwenye ujenzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Maombi upimaji wa DNA yaongezeka

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imesema inapokea maombi 10 hadi 15 kwa mwezi ya wazazi kupima vinasaba (DNA) kubaini uhusiano wa baba na watoto.

Fundi Sanifu Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Rashidi Mjema, alitoa takwimu hizo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya nne ya Viwanda Vidogo (SIDO), mkoani Njombe.

Alisema uhitaji wa kupima vinasaba DNA ni mkubwa kutokana na udanganyifu unaotokea kwa wanandoa kubambikia kinababa watoto.

"Lakini hii pia ni kwa kinababa ambao wanakataa majukumu yao pia ni wengi kwa hiyo uhitaji huu ni mkubwa sana kwa sasa hivi," alisema Mjema.

Mjema alisema kuwa huduma hiyo si ya kumtambua baba wa mtoto pekee, bali ni teknolojia mbayo inabaini wahalifu katika matukio mbalimbali ikiwamo ujambazi.

"Kwa kushirikina na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya sheria ni maabara hii pekee inatumia hii teknolojia na kutatua kesi mbalimbali, sasa tukija katika DNA ya mahusiano ya baba na mtoto ambayo wengi wanaihitaji katika nchi hii, namaanisha kujua baba halali wa mtoto wengi huwa hawafahamu hizi taratibu zetu," alisema Mjema.

**UTARATIBU WA KUPIMA**

"Taratibu ni rahisi tu mteja atatakiwa apitie ustawi wa jamii au kwa mwanasheria anayetambulika au kwa mahakama, akishakuja na barua basi tutamtengenezea namba ya malipo ambayo ni Sh. 300,000, kwa baba, mama na mtoto tutachukua kipimo halafu atasubiri takribani siku 21 hadi 30 za kazi, tutampatia majibu yake huo ndio utaratibu mwepesi ambao tunautumia kwa wale ambao wanachangamoto ya kujua uhalali wa baba wa mtoto," alisema Mjema.

Kipimo cha DNA pia hufanyika kama mtu anataka kubaini uhalisi wa uhusiano wake na ndugu zake wa mbali wakiwamo bibi, babu, binamu na wengine.

Kwa mujibu wa taarifa za mtandao, vile vile, kipimo cha DNA humsaidia mtu kutambua kama ana hatari ya kupata maambukizo ya ugonjwa kwenye mwili wake.

Taarifa mbalimbali zinaeleza kuwa watu walio kwenye ndoa hasa wanaume wana uwezekano mkubwa wa kulea watoto ambao si damu zao kutokana na kubambikiwa na wenza wao.

Hali hiyo hujitokeza kama mmoja kati yao, hasa mwanamume anapokuwa hana uwezo wa kuzalisha mbegu zinazomwezesha mwanamke kushika ujauzito.

Taarifa zinasema wanaume sio wepesi kwenda hospitali kujua hali zao kiafya kama ilivyo kwa wanawake na matokeo yake hulea watoto ambao si wa kwao kwa madai kuwa wanawake kulinda heshima za waume zao ndani ya ndoa.

Mkemia daraja la pili kutoka Wakala ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ruben Sendelema, alizungumzia madhara ya sumu kuvu kwamba ni aina ya sumu inayopatikana kutoka kwa jamii aina ya fangasi ambao wao wanaathiri mazao kama vile nafaka zikiwamo mahindi, mchele na karanga.

"Sumu kuvu inaweza ikaathiri mazao kwa njia tofauti tofauti ikiwamo mkulima wa mazao hakufuata taratibu zinazotakiwa mpaka kufikisha mazao katika hali ambayo ni ya uhifadhi kwa mfano kiasi cha unyevunyevu kisipozingatiwa katika mazao inaweza ikasababisha wale fangasi wakajitokeza," alisema Sendelema.

Alisema mazao yaliyoathiriwa na sumu kuvu yakiliwa na binadamu yanasababisha madhara mbalimbali kama kansa na kuwataka wananchi kujihadhari na tatizo hilo.

bgtl **BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na NMB BANK PLC Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA**.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | YUSUPH MBOETO | Nyumba ya makazi iliyopo Mabibo Sahara yenye leseni ya makazi KND/MBB/MBO16/114 Manispaa Ya Ubungo | 15.11.2023 | ILALA |
| 2. | ALEX CHACHA AMOS | 1.Nyumba Ya Makazi Iliyopo Yombo Vituka Yenye Leseni Ya Makazi TMK/YBV/BMW25/71 Manispaa Ya Temeke.<br>2. Nyumba Ya Makazi Iliyopo Manzese Yenye Leseni Ya Makazi MZS/MNM/425 Manispaa Ya Ubungo. | 18.11.2023<br>02.12.2023 | ILALA |
| 3. | ABILAH HASSAN MATENDE | Nyumba Ya Makazi Yenye Hati Ya Mauziano Iliyopo Majohe Rada Shehe Juma Mosque Manispaa Ya Ilala. | 22.11.2023 | BANK HOUSE |
| 4 | TENTONE IMAGING TECHNOLOGY/KUMBUKA DEUS NTEJA | Nyumba Ambayo Haijakamilika Iliyopo Kigogo Kati Yenye Leseni Ya Makazi KND/KGG/KSTII/82 | 15.11.2023 | ILALA |
| 5 | ZAHARA HUSSEIN | Nyumba Ya Makazi Iliyopo Kwenye Kiwanja Chenye Leseni Ya Makazi Maeneo Ya Mangaya Mbagala TMK/MBGL/MANII/269A Manispaa Ya Temeke | 18.11.2023 | MBAGALA |
| 6 | BENSON NAHUM BAREGE | 1.Nyumba Ya Makazi Yenye Kipande Cha Ardhi Na TMK/MBGL/KZG5/299 Yenye Leseni No TMK032/02 Iliyopo Kizinga Manispaa Ya Temeke<br>2.Nyumba Ya Makazi Yenye Kiwanja No 28 & 29 Kitalu H Leseni Na 139102 Na No 551610 Iliyopo Chamazi Manispaa Ya Ilala | 25.11.2023<br>25.11.2023 | B/CENTER |
| 7. | JOHN JOSEPH LUHAZI | Nyumba ya Makazi ,Iliopo Tegeta kwa Ndevu Mtaa wa Msichoke, Manispaa Ya Kinondoni | 29.11.2023 | TEGETA |
| 8. | DOSTEA PHARES NYABENDA | Nyumba ya Makazi ,Iliopo Tegeta kwa Ndevu Mtaa Wa Msichoke, Manispaa Ya Kinondoni. | 29.11.2023 | TEGETA |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na: AU**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD .**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**Email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

# Majaliwa ataka kasi udhibiti magendo viwanja vya ndege

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, ametoa maelekezo saba kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kuimarisha mifumo ya udhibiti wa matumizi mabaya ya viwanja kwa kuhakikisha havigeuki kuwa uchochoro wa kupitisha bidhaa haramu.

Pia ameagiza Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kufanya marejeo kuona namna ya kufadhili mafunzo ya urubani kwa kutoa kipaumbele kwa wahitaji wa fani za usafiri wa anga.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa TCAA mwaka 2003.

"Hakikisheni viwanja vyetu haviwi uchochoro wa usafirishaji bidhaa haramu ili nchi yetu iendelee kuwa na sifa kati ya nchi zenye udhibiti wa usafiri wa anga," alisema.

Majaliwa pia alisema gharama za vyuo kusomea masomo ya urubani au fani za masuala ya anga ni kubwa, hivyo jamii inashindwa kumudu gharama, hivyo ikiwekwa huduma hiyo, watapata watu wengi.

Aidha, Majaliwa aliwataka wadau wote wa usafiri wa anga nchini kutekeleza majukumu yao kwa kufuata kanuni, sheria, taratibu na miongozo inayosimamia tasnia hiyo kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuhakikisha usalama ni kipaumbele cha kwanza.

Pia aliwataka watendaji wa TCAA kufanya kazi kwa weledi na ubunifu ili kumudu soko la ushindani katika utoaji huduma za anga kwa kuhakikisha wanajifunza kutoka katika mataifa mengine.

"Tujifunze katika mataifa mengine yaliyofanikiwa ili kuongeza viwango vyetu vya kutoa huduma nzuri na zenye ubora zaidi," alisema Majaliwa huku akiitaka TCAA kubuni na kuongeza vyanzo vipya vya mapato ya 'Avition Training Fund', ili kuongeza idadi ya marubani wanaopata ufadhili wa masomo.

Kadhalika, aliwataka Watanzania kuendelea kuviamini na kutumia vyuo vya nchini vinavyotoa mafunzo ya utaalamu wa anga, kwa kuwa vina uwezo mkubwa na vinaaminika barani Afrika.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisemaTanzania imefanikiwa kushika nafasi ya nne barani Afrika kwenye masuala ya usalama wa anga kwa kupata alama 86.7 ikitanguliwa na Nigeria, Kenya na Ivory Coast katika ukaguzi uliofanyika Mei, 2023.

"Kwenye ukaguzi mwingine wa uwezo wa nchi kiusalama uliofanywa na Shirika la ICAO, viwanja vya ndege vya KIA, Zanzibar na JNIA Dar es Salaam vilikaguliwa na kupata alama 86.7.

"Hatua hii, imewezesha nchi kushika nafasi ya nne Afrika ikitanguliwa na Nigeria, Kenya na Ivory Coast. Huu ni ushahidi tosha kwamba uwezo wa nchi yetu katika kudhibiti usalama wa anga unaendelea kuimarika," amesema.

Waziri Mkuu ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye ufunguzi huo, alisema Tanzania imeongeza uwezo wa udhibiti wa sekta ndogo ya usafiri wa anga nchini kwa viwango vya kimataifa.

"Kupitia kaguzi za Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO), sekta ndogo ya usafiri wa anga nchini, imeongeza uwezo kutoka asilimia 37.8 mwaka 2013 hadi asilimia 69.04 mwaka 2019. Kutokana na ufaulu huo, ICAO imetoa ufadhili wa dola za Marekani milioni moja ambazo zilitumika kwenye mradi wa kuendelea kuboresha uwezo wa usimamizi wa anga letu."

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni ongezeko la mchango wa sekta ya uchukuzi katika Pato la Taifa, huku akibainisha kuwa katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo, sekta hiyo ilichangia asilimia 8.2 ya pato la Taifa kwa mwaka 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, alisema wakiwa wanaadhimisha miaka 20 wamepiga hatua kubwa ikiwamo kushika nafasi ya nne barani Afrika.

Alisema usalama ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa majukumu yao katika kuhakikisha anga linakuwa salama na mwaka 2017, serikali iliridhia ununuzi wa rada nne za kuongoza ndege za kiraia.

Johari alisema jukumu lao ni kuhakikisha sekta ya usafiri wa anga ina wataalamu wa kutosha na wenye utaalamu stahiki unaoendana na viwango vya kimataifa kwamba kwa sasa wana marubani 603.

# Ripoti CAG, Bima ya Afya kwa Wote kulitikisa Bunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUTANO wa 13 wa Bunge unaanza leo vikao vyake jijini Dodoma huku wabunge wakitarajiwa kujadili ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.



Sambamba na mjadala huo kusubiriwa kwa hamu na Watanzania, pia bunge hilo litajadili Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Katika mkutano huo, mambo mengine yatakayojadiliwa ni taarifa za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu hesabu zilizokaguliwa na CAG kwa mwaka 2021/22 na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, licha ya kuwekwa kwenye ratiba ya mkutano wa bunge wa Februari, mwaka huu, kwa ajili ya kusomwa kwa hatua zote tatu za mchakato wa utungwaji sheria, uliondolewa kutokana na kuwapo na maoni mbalimbali ambayo serikali iliamua kuyafanyia kazi.

Aidha, Bunge litapokea na kujadili maelezo ya serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Aidha, Bunge linatarajiwa kupokea, kujadili na kuridhia Azimio la Bunge la Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Dawa ya Afrika wa Mwaka 2019.

Pia litajadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2023 na Muswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa Mwaka 2023.

# ACT yavunja ukimya kushiriki uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama chake kitashiriki uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na uchaguzi mkuu mwaka 2025 hata kama hakutakuwa na Katiba Mpya.

Zitto alisema hayo juzi wakati akihojiwa katika kipindi cha 'Medali za Siasa' kinachorushwa na kituo cha televisheni cha Star TV.

"Sisi si chama cha ajenda moja, tutashiriki chaguzi (uchaguzi) zote zinazokuja (unaokuja) katika mazingira yoyote. Miaka hii mitatu ya bunge la chama kimoja tumeshuhudia masuala ya wananchi hayajadiliwi bungeni.

"Hatuwezi kumwacha nguruwe kwenye shamba la mihogo, atamaliza yote shambani. Chama chetu kitashiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwaka 2025 ili kupata wawakilishi wa kusaidia jamii bila kujali mchakato wa Katiba umefikia hatua gani," alisema.

Msimamo huo wa ACT- Wazalendo ni tofauti na wa baadhi ya vyama vya siasa kikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ambacho kwa nyakati tofauti kupitia kwa viongozi wake wakuu, kimekuwa kikitoa matamko yenye kigugumizi kuhusu kushiriki katika uchaguzi ukiwamo uchaguzi mdogo kama ambavyo ACT-Wazalendo imekuwa kikishiriki kwa madai kuwa sheria zinazosimamia uchaguzi huo si rafiki katika kuendesha uchaguzi wa uhuru na haki.

Akijibu swali aliloulizwa kuhusu chama hicho kuitwa CCM B, Zitto alisema hizo ni propaganda za kawaida na hawajali kuhusu hilo.

"Hizo ni propaganda za kawaida za kisiasa. Wakati NCCR Mageuzi na CUF vikiwa vyama vikubwa vya upinzani nchini, waliwaita CHADEMA kuwa ni CCM B kwa kuwa kilikuwa chama kidogo.

"Lakini CHADEMA ilipofanya vizuri nayo ikaanza kuwaita NCCR Mageuzi na CUF kuwa ni CCM B, hivyo sioni taabu hata kidogo na sisi kuitwa hivyo. Muhimu ni sisi kusimama kwenye reli kwa yale ambayo tunayasimamia, ufanyaji siasa hauwezi kufanana na wa kwao," alisema huku akisisitiza kuwa chama kipo kwa ajili ya kuzungumzia masuala yote ya wananchi.

"Sisi si chama cha ajenda moja ndiyo maana tunazungumzia masuala yote ya wananchi. Sisi siyo chama cha kupiga kelele na kubwabwaja bwabwaja. Inapotokea changamoto ya kitaifa utatuona, hatuishii kusema tu bali tunapendekeza namna ya kufanya na kuna muda serikali inatekeleza kile tunachopendekeza," alisema Zitto.

Akitolea mfano suala la uwekezaji wa Bandari, Zitto alisema mapendekezo mengi yaliyotolewa na chama hicho yamechukuliwa.

"Kwenye suala hilo la uwekezaji wa bandari, chama kilikosoa kwa njia ya kutoa majawabu kwa sababu tunafahamu umuhimu wake. Watu wengi walikuwa wanaongea na kutoa maoni, baadhi walikuwa hawaelewi nafasi ya uchumi wa jiografia katika kukuza uchumi wetu. Sisi tuliona kwamba Bandari inaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

"Kwa hiyo tuliona tupendekeze mambo ambayo yalikuwa yanaleta ukakasi wa mambo ambayo yamekuwa yakizungumzwa kuhusu makubaliano kati ya serikali yetu na Emirates ya Dubai na mengi tuliyoyapendekeza yamechukuliwa, kati ya matano tuliyopendekeza, yamechukuliwa manne," alisema.

"Na hiyo inakuonyesha faida ya siasa za masuala mbalimbali kwamba unaweza ukabadilisha nchi bila kuwa madarakani na huo ndio uongozi. Uongozi siyo cheo tu," alisisitiza.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa Mafundi Sanifu, Wanawake na Vijana kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Mafunzo haya yatafanyika katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo Yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Mafundi Sanifu, Vikundi vya Wanawake na Vijana katika Ukarabati na Matengenezo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)**<br>20/11/2023 – 17/12/2023 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbali mbali kuhusu ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na mada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya Barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kuwezesha Wanawake na Vijana (washiriki) kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; Awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na Awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali kuhusu matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani **"SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS"** kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na **TARURA** au **TANROADS.**

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

a) Walengwa wa mafunzo haya ni kwa makundi Maalumu ya Wanawake na Vijana amabao wana azma ya kuwa wajasiriamali.
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka ZANROADS – Zanzibar.
c) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**
**Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Uhangarawe/Udongo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana**
i. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi atalipa ada kiasi cha Tsh. 700,000.

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu: 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu: 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

# Kinana ashangaa baadhi viongozi kutoheshimika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdurahaman Kinana, amesema kuna watu wana vyeo vikubwa lakini hawaheshimiwi na wengine hawana vyeo, wala hawajasoma wanaheshimika kwa sababu ya tabia njema.

Akitoa salamu za rambirambi za chama hicho jana katika maziko ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Zelothe Steven, Kinana alisema kwa kuwa maisha ni hadithi, hivyo kila mmoja ni vizuri akaishi kwa kuwekeza kwenye tabia njema.

Zelothe ambaye aliwahi kuwa Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) na kuhudumu katika mikoa mbalimbali katika nafasi ya kamanda wa polisi wa mkoa, alizikwa nyumbani kwake, Kijiji cha Olosiva, Arumeru mkoani Arusha.

"Marehemu Zelothe alikuwa mnyenyekevu, mwadilifu, muungwana, msikivu na mpenda kujenga umoja na japokuwa alikuwa na vyeo vingi vikubwa. Aliishi kwa unyenyekevu bila kujali vyeo alivyo navyo," alisema na kuongeza kuwa watu walimheshimu sio kwa vyeo vyake vikubwa vya kipolisi na serikali, bali kwa tabia yake kwa watu alioishi nao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussen Mwinyi, alisema Zelothe ni kiongozi aliyeacha alama kwa taifa.

Katika ibada ya maziko ya Zelothe, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Solomon Masangwa, alisema Zelothe alikuwa muumini mwadilifu, mpenda watu na alipenda kufanya kazi za kanisa.

Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, Mkuu wa Operesheni na Mafunzo, Kamishna (CP) Awadhi Haji, alisema wamepokea taarifa za kifo hicho kwa masikitiko makubwa kwa sababu Zalothe alikuwa mwadilifu ndani ya jeshi hilo na walishirikiana naye kwenye masuala mbalimbali ya ulinzi na usalama wa nchi. Alisema alifanya kazi kwa weledi mkubwa, nidhamu haki na uadilifu mpaka alipostaafu.

**WASIFU WAKE**

Akisoma wasifu wa marehemu, mmoja wa watoto wake, Wille Stephen alisema Zelothe alizaliwa Novemba 30, 1950 katika Kijiji cha Ilkiranyi, Arumeru akiwa mtoto wa pili katika familia ya Stephen Oldarasu na Dina Oldarasu yenye watoto tisa kati yao watoto watano wakiume na wanne wakike.

Alisema Zelothe alimaliza elimu ya msingi katika Shule ya Mringa, wakati huo Mringa "Upper Primary School" mwaka 1966 na baadaye alijiunga na elimu ya sekondari katika shule ya Enaboishu mkoani Arusha na kuhitimu kidato cha nne mwaka 1968.

Baada ya hapo, alijiunga na Chuo cha Mafunzo ya Jeshi la Polisi katika Chuo cha Polisi Moshi na kuhitimu mwaka 1970.

Aliendelea na mafunzo mbalimbali yakiwamo ya usalama barabarani, uongozi, kupambana na uhalifu na kutokana na juhudi zake za kupenda kusoma, alichukua mafunzo nchi za nje ikiwamo Japan (1998 -2000), Marekani (2001 na 2007), Ujerumani (2005) na Uingereza mwaka 2008.

Katika mazishi hayo viongozi mbalimbali wa CCM taifa, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na serikali ngazi ya kitaifa, walishiriki. Mbali na Kinana, wengine waliohudhuria ni Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Paul Makonda.

Zelothe alifariki dunia Oktoba 26, mwaka huu, katika Hospitali ya Emilio Mzena, Dar es Salaam, wakati akipatiwa matibabu.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamilla (wa tatu kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Kidakio cha Pwani, Halima Paraji (wa pili kulia), katika hafla ya uzinduzi wa kitalu cha miti rafiki, vyanzo vya maji na miti ya matunda Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu Tawala Wilaya ya Ubungo, Hassan Mkwawa na kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Bonde la Wami na Ruvu, Martin Kasambala. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mwinyi asisitiza uadilifu vikosi vya ulinzi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amevitaka vikosi vya Serikali Zanzibar kuendeleza uadilifu na uwajibikaji wa majukumu yao ya kila siku.

Dk. Mwinyi ambaye ni Kamanda Mkuu wa Idara Maalum ya vikosi vya SMZ, alisema hayo, alipokuwa akizungumza na wapiganaji kwenye viwanja vya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa lengo la kuwapongeza kutokana na juhudi zao za kuhakikisha amani na utulivu nchini vinaendelea kuimarishwa.

Alivitaka vikosi hivyo kuweka mbele maslahi ya nchi kwanza, uwajibikaji pamoja na kusimamia uadilifu jeshini.

Alivisisitiza vikosi hivyo suala la kusimamia nidhamu kwenye maeneo yao ya kazi ili kufanya kazi zao kwa uadilifu.

"Nidhamu ikikosekana katika jeshi basi hapo hakuna jeshi," alisema Rais Dk. Mwinyi.

Pia, alivipongeza vikosi hivyo kwa jitihada zao za kutoa huduma bora kwa jamii kikiwamo Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kupitia hospitali yao iliyopo Bububu pamoja na Hospitali ya JKU, Saateni kwa huduma za afya wanazozitoa kwa wananchi na nyingine za jamii vikiwamo vyuo vya amali na taaluma.

Alivitaka vikosi hivyo kuwa mfano mzuri wa kutoa huduma bora kwa raia hasa kwenye vituo vyao vya afya na taaluma vinavyohudumia jamii.

Aliwaagiza wakuu wa vikosi hivyo kuendelea kusimamia uwajibikaji ili kuwe na tofauti baina ya hospitali za jeshi na za raia ili wananchi wapate huduma bora.

Pia Dk. Mwinyi alivieleza vikosi hivyo kuwa vinajukumu la kutoa malezi bora kwa vijana na kuhakikisha wanatoa vijana wazalendo wenye uchungu wa nchi yao watakaopigania maslahi ya taifa lao.

Akizungumzia suala la kuwajengea uwezo maofisa na wapiganaji wa vikosi hivyo, Rais Dk. Mwinyi aliwataka wakuu wa vikosi hivyo kuwaongezea uwezo wa kitaaluma maofisa hao kwa kuwapatia fursa za mafuzo.

Waziri wa Idara Maalum ya Vikosi vya SMZ, Masoud Ali Muhammed, alisema, vikosi vya SMZ idara zote tano ziko tayari kuendeleza jukumu mama la kuimarisha na kuendeleza amani, utulivu na mshikamano uliopo nchini vinaendelea kusimama wakati taifa likiendeleza maendeleo ya watu wake.

Akiwasilisha risala ya vikosi vitano vya Idara Maalum ya SMZ, Katibu Mkuu wa Idara hiyo, Issa Mahafoudh Haji, alisifu juhudi kubwa ya Kamanda Mkuu wa Idara Maalum ya vikosi vya SMZ, Rais Dk. Mwinyi aliyoifanya kwa vikosi hivyo.

Alimshukuru Rais Mwinyi kwa kuvishirikisha vikosi hivyo kwenye ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo nchini na kueleza kuwa imewaongezea uwezo na nguvu za kiuchumi kwa kutatua baadhi ya changamoto zao.

Pia, alisema ushiriki wao kwenye miradi hiyo, umepanua uwezo wao wa ufahamu na ujuzi wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku pamoja na kusifu hatua ya kuwapandishia mishahara makamanda na wapiganaji kutokana na nyongeza ya mishahara aliyoitoa kwa watumishi wa umma wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinaundwa na Jeshi la kujenga Uchumi (JKU), (KMKM), Vikosi vya Uokozi na Zimamoto, Valantia (KVZ) na Chuo cha Mafunzo.

# Tulia asimulia magumu aliyopitia urais wa IPU

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameeleza ugumu na wepesi aliopitia hadi kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Oktoba 27, mwaka huu, Luanda nchini Angola.

Dk. Tulia alisema hayo jana kwenye hafla ya kumpongeza kwa kuchaguliwa katika nafasi hiyo na kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika kushika wadhifa huo, iliyofanyika kwenye viwanja vya Bunge, jijini hapa.

Alisema uchaguzi huo ulikuwa mgumu kutokana na mitandao ya kijamii kutumika kumchafua ili asichaguliwe.

"Uchaguzi ule ulikuwa mgumu sana na hii ni kutokana na mitandao ya kijamii kutumika kunichafua. Tena waliofanya hivyo ni Watanzania wenzetu ambao walikuwa wanaungana na watu wengine ili tu nisishinde kwenye nafasi hii.

"Ni jambo la ajabu sana Watanzania kuungana na adui zetu kulipiga vita taifa letu. Niwaombe linapotokea suala la kitaifa tuwe kitu kimoja badala ya kuungana na adui zetu kuumizana wenyewe kwa wenyewe," alisema.

Pia alisema makubaliano ya awali yalikuwa mataifa mengine katika Afrika yasiweke wagombea ili kuiunga mkono Tanzania lakini kutokana na maneno ya mitandao ya kijamii, nchi zingine zilipata nguvu ya kuingiza wagombea wao.

"Nchi nyingi zilisema hazitaingiza wagombea na kuipa nafasi Tanzania lakini sasa maneno ya kwenye mitandao yaliwapa nguvu ya kuleta wagombea. Lakini kwa kuwa Mungu alikuwa amepanga Tanzania ishinde, hakuna kilichobadili hilo," alisema.

Alibainisha kuwa watu ambao walikuwa wanaichafua Tanzania na mgombea wake baadhi ni viongozi ambao waliwahi kushika nafasi katika nyadhifa za juu za kitaifa.

"Mimi ninaposemwa huwa nafurahi sana lakini kwa hili huyo mmoja lazima nimtafute ili nijifunze kutoka kwake maana yake hawezekani mtu aliyewahi kuwa kiongozi wa juu kuungana na adui kuichafua nchi yetu. Lazima watu tuweke utaifa kwanza si tu kwa sababu una bando basi unazungumza kila unachokiona," alisema.

Pia alisema mambo ambayo yamemsaidia kushinda uchaguzi huo ni kuungwa mkono na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alimpa kibali cha kuingia katika kinyang'anyiro hicho.

"Rais amekuwa mstari wa mbele kuitangaza diplomasia ya taifa letu kwa mataifa mengine na yeye mwenyewe kushiriki katika kunipigia kampeni kwa mataifa mengine hali ambayo ilifanya baadhi ya wajumbe kuja na maagizo kutoka katika serikali zao," alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alimpongeza Dk. Tulia kwa kushinda katika uchaguzi huo na kumwahidi kuwa serikali itampa ushirikiano wa kutosha wakati wote atakapo uhitaji.

"Nafasi hii itakupa fursa ya wewe kushiriki vikao vyote vya UN hivyo na sisi kama taifa tutakutumia wewe kupenyeza ajenda zetu hivyo kwa niaba ya Rais tunakuahidi kukupa ushirikianao wa kutosha kila utakapohitaji," alisema Majaliwa.

Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, alisema Dk. Tulia anakuwa Rais wa 31 wa IPU na mwanamke wa tatu kushika nafasi hiyo lakini anakuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika na ataongoza umoja huo kwa kipindi cha miaka mitatu.

**TANGAZO**

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 30/09/2023 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2023 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 86 | 61 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 8,801 | 6,047 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | | - | - |
| | Mikopo Halisi Iliyopo | 37,058 | 32,969 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,725 | 2,595 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 2,064 | 1,853 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **50,735** | **43,524** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 4,402 | 4,187 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3,052 | 3,004 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 13 | 12 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mte | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 1,052 | 193 |
| 27 | Zitakazolipwa Baadae | 3,905 | 3,312 |
| 28 | Dhima Nyingine | 14,628 | 9,250 |
| **29** | **Madeni** | **27,051** | **19,957** |
| | **JUMLA YA DHIMA** | | |
| **30** | **MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **23,684** | **23,567** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,537 | 1,537 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (2,401) | (2,401) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,180 | 996 |
| 35 | Akauti Nyingine za Mtaji | 2,167 | 2,235 |
| **36** | **Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **23,684** | **23,567** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | **692** | **611** |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **993** | **927** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **47%** | **54%** |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **1.9%** | **1.8%** |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **499%** | **471%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **73%** | **78%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **83%** | **85%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **3.7%** | **3.2%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **16.6%** | **14.2%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30/09/2023 | Robo ya Mwaka Linganishi 30/09/2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 4,355 | 2,670 | 12,222 | 7,571 |
| 2 | Gharama za Riba | 428 | 10 | 1,053 | 21 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **3,927** | **2,661** | **11,169** | **7,550** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (253) | **(206)** | (560) | **(450)** |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,254** | **780** | **3,238** | **2,075** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 71 | (27) | 276 | (43) |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 771 | 522 | 2,162 | 1,501 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 412 | 285 | 801 | 618 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba :** | **4,744** | **6,118** | **12,667** | **12,544** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,195 | 1,594 | 6,315 | 4,513 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 2,548 | 4,523 | 6,351 | 8,032 |
| | 7.3 Ada na Kamisheni | | | | |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **184** | **(2,883)** | **1,180** | **(3,369)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10** | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **184** | **(2,883)** | **1,180** | **(3,369)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **438** | **352** | **438** | **352** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 8,692 | (135,981) | 55,684 | (158,937) |
| 13 | Kipato kwa Hisa | 8,692 | (135,981) | 55,684 | (158,937) |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 35 | 54 | 35 | 54 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 0.4% | -9.2% | 2.5% | -10.7% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.8% | -13.0% | 5.0% | -15.3% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 92% | 178% | 88% | 130% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalish | **20%** | **22%** | **57%** | **62%** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 13 Octoba 2023 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | | 13 Octoba 2023 |
| Modest Kissima (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 13 Octoba 2023 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 **Athanasia Soka ( Mwenyekiti ya Bodi)** | | 13 Octoba 2023 |
| 2 **Loyce Isanzu (Mwendeshaji)** | | 13 Octoba 2023 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/09/2023 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **I:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **184** | **730** | **1,180** | **(3,369)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 140 | 91 | 394 | 469 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (4,090) | (2,927) | (9,149) | (3,533) |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 263 | 220 | 549 | 131 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (131) | (321) | (552) | (158) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | 1,453 | (135) | 375 | 2,306 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **(2,181)** | **(2,341)** | **(7,202)** | **(4,155)** |
| **II:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | | | | |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (350) | (306) | (920) | (482) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za uekezaji** | **(350)** | (306) | (920) | (482) |
| | | - | - | - | - |
| **III:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **5,378** | 4,632 | 10,010 | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | 1,146 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (68) | (35) | 283 | (1,882) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **5,311** | **4,597** | **11,440** | **(1,882)** |
| **IV:** | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | | | | |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tast | 2,779 | 1,951 | 3,318 | (6,518) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwa | 6,108 | 4,157 | 5,569 | 10,754 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu / Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **8,887** | **6,108** | **8,887** | **4,236** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2023)** | **21,200** | **(2,418)** | **0** | **2,292** | **21,074** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **1,180** | - | - | **1,180** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **17** | - | **1,412** | **1,429** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **21,200** | **(1,220)** | **0** | **3,704** | **23,684** |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2022)** | **21,200** | **2,487** | **0** | **2,124** | **25,811** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **(3,260)** | - | - | **(3,260)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **(1,645)** | - | **168** | **(1,477)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **(2,418)** | **0** | **2,292** | **21,074** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

| | Huduma za Kibenki | | Gharama-Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani & ATM | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | Ndani ya VFT hadi TZS1,000,000 | 944 |
| | | Ndani ya VFT zaidi ya TZS1,000,000 | 1,180 |
| | | Kwenda Benki nyingine hadi TZS10,000,000 | 3,554 |
| | | Kwenda Benki Nyingine zaidi ya TZS10,000,000 | 11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi TZS 5,000,000 | | 1,770 |
| 4 | Kutoa ATM | | 1,500 |
| 5 | Kadi ya ATM (Mpya au Kubadili) | | 5,000 |
| 6 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Akaunti | 885 |
| | | Business Akaunti | 1,770 |
| 7 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | 2,360 |
| | | Akaunti ya Vikundi na Biashara | 5,900 |
| 8 | Taarifa ya Akaunti | Taarifa Fupi ATM | 720 |
| | | Miezi 0-3 | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | 55,400 |

| | Huduma Za Simu (Mobile banking) | Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|
| 9 | Kujua Salio-Simu | 118 |
| 10 | Kutoa-Simu | Bure |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | 236 |

**Akaunti**

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka * |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Akaunti | 5,000 | 3% |
| 2 | Salary Akaunti | 5,000 | 3% |
| 3 | Kikundi Akaunti | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Akaunti | 10,000 | 4% |
| 5 | Bussiness Akaunti | 100,000 | 3% |
| 6 | Joint Akaunti | 5,000 | 3% |
| 7 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 8 | Dunduliza Accounts | 10,000 | 4% |

** Riba kwa akaunti za aina zote itajilimbikiza kwa kila la siku kwa kiasi cha akiba cha TZS100,000 na kuendelea na kulipwa kila Mwezi.*

**Mikopo ya Vikundi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mikopo ya Vikundi -Biashara group Loan | 5% | 60% | 3% |
| 2 | Mikopo ya Vikundi/Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% |
| 3 | Mikopo ya Vikundi -Jiendeleze Group Loan | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo Binafsi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% |
| 5 | Mkopo Binafsi inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% |
| 6 | Mikopo Binafsi inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo ya Kilimo**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Mikopo Binafsi -Jikomboe Loan | 4% | 48% | 5% |
| 10 | Mikopo ya kikundi -Jitume | 5% | 60% | 5% |
| 11 | Mikopo ya Kikundi -Mkombozi Loan | 5% | 60% | 5% |
| 12 | Patnerships | Negotiable | Negotiable | Negotiable |

| Name and Title | Signature | Date |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma ( Chief Executive Officer) | Signed | 13/Oktoba/2023 |
| Rogathe Godson (Chief Finance Officer) | Signed | 13/Oktoba/2023 |
| Modest Kissima ( Internal Audit Manager) | Signed | 13/Oktoba/2023 |

217882001

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukusanyaji taka uzingatie ratiba kuepuka mrundikano

**TATIZO** la uzoaji taka katika miji mingi nchini linasababisha taka kuzagaa na kuchafua mazingira.

Mitaa mingi ambayo imeweka utaratibu wa kuzoa taka kwa kutumia magari ya makandarasi, ratiba hazizingatiwi hali inayofanya taka kuendelea kurundikana na kuzagaa.

Uchafu unapozidi husababisha uchafuzi wa mazingira na vile vile harufu kali inayotokana na uchafu huo.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alitoa angalizo kwa mkoa wake kuwa tatizo la uondoshaji taka mkoani humo ni kubwa na linadumaza viwango vya usafi.

Mkuu huyo ametafuta ufumbuzi wa mkoa kuunda kitengo maalumu cha ukusanyaji taka.

Mfumo huo utakabidhiwa kwa mkandarasi mmoja badala ya ilivyo sasa wanatumika makandarasi tofauti kufanya shughuli hiyo mitaani na kutokuwapo kwa ufanisi na ufuatiliaji.

Usimamizi duni pia eneo la ukusanyaji taka katika madampo umeelezwa unaathiri madampo hayo hasa kwa baadhi ya magari yanayoendesha shughuli katika eneo hilo kuibwa.

Pia imefahamika kuwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutupwa taka (dampo) yanaonekana kuelemewa na taka, kiasi taka hizo kuzagaa na kuleta athari kwa wakazi wanaoishi eneo karibu na dampo.

Kwa mfano Juni, mwaka huu, gazeti hili lilifika eneo la dampo la Pugu Kinyamwezi, Jiji la Dar es Salaam na kubaini kasoro kadhaa, kama kujaa kwa dampo, kutokuwapo kwa magari maalum (buldoza) ya kusambazia taka na utoroshwaji mafuta na malori yanayofikisha taka eneo hilo kukaa saa nyingi kwenye foleni.

Baadhi ya wafanyakazi binafsi wanaofanya kazi katika dampo hilo, ikiwamo madereva wa malori yanayowasilisha taka kwenye dampo hilo, walikiri ugumu wa kazi kutokana na foleni ndefu inayowalazimu kutumia siku nzima hadi kukamilisha kazi ya kumwaga taka.

Tatizo lingine linalokwamisha uzoaji taka kutofanyika kwa ufanisi ni watu kutokuwa waaminifu. Suala la uibaji mafuta kwenye magari yanayokwenda kuzoa taka hizo si jambo la kuliacha liendelee.

Mafuta yanapoibwa hizo taka zitazolewaje wakati vitendea kazi vinakosa rasilimali ya kufanyia kazi.

Ndio maana kwenye maeneo mengi wananchi wanakusanya taka na kuzijaza kwenye viroba na kwenda kuzitupa barabarani.

Kwa mfano Jiji la Dar es Salaam limebeba taswira ya nchi ikiwamo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), linapokuwa chafu na wageni wanaingia na kupokewa na harufu ya taka au kukuta taka hizo zikiwa barabarani haileti picha nzuri.

Mkoa wa Dar es Salaam, unakadiriwa kuzalisha taka takribani tani 5,600 kwa siku huku asilimia 45 hadi 50 pekee ndizo hudhibitiwa na kupelekwa katika dampo la Pugu Kinyamwezi, linalotegemewa na mkoa mzima, kutoka wilaya tano za mkoani humo.

Mkoa una wilaya tano; Kigamboni, Ilala, Ubungo, Temeke na Kinondoni, kiwango cha uzalishaji taka hutofautiana, huku mzigo mkubwa ukiwa Halmashauri ya Ilala ambako taka zinapokewa katika dampo la Pugu Kinyamwezi.

Kukua kwa jiji na idadi kubwa ya wakazi inayofikia milioni 5.4 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, kumeongeza changamoto ya uondoaji taka maeneo ya makazi, masoko na ofisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Tusilee watoto wetu kwa simu

**IMEIBUKA** tabia ya wazazi na walezi ya kuwapa watoto wao wadogo simu za mkononi wakiamini kwamba ni malezi bora licha ya kufahamu kuwa wanawaharibu.

Mara nyingi utawasikia wengi wao wakisema simu janja au za kupangusa zinasaidia kuwatuliza na kuwabembeleza wasiwasumbue wala kulia wakati wakiendelea na shughuli zao iwe nyumbani au popote.

Mara kwa mara wazazi na walezi hao wamekuwa wakisikika wakiwasifia watoto wao jinsi walivyo mahiri kutumia simu hizo, kwa kufungua picha, katuni, kusikiliza muziki, kucheza 'gemu' na vitu vingine mbalimbali vilivyomo kwenye simu hizo, wakionyesha ufundi hata kuliko watu wazima.

Waswahili husema mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, siyo siri wengi tumekuwa mashuhuda kwenye makazi yetu, mtoto anavyomuanda mzazi, mlezi hata awe mgeni amekwenda nyumbani kwao, akikimbilia kukwapua simu na kuanza kubofya bofya, kuweka anachotaka na wakati mwingine akipiga huku akiita haloo haloo.

Badala ya mzazi au mlezi kumkemea utakuta anamsifia akisema mtoto huyu bwana anapenda simu kwa ajili ya kumpigia baba au mama yake anapokuwa kwenye shughuli zake za kusaka 'tonge'. Anazidi kutangaza kwa marafiki kuwa mtoto wake bila kumpa simu analia, kususa kula na wakati mwingine anagoma kulala.

Tumewasikia wenyewe wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wameibuka na kuonya baada ya kubaini kuwa tabia hiyo imezidi kuota mizizi miongoni mwetu.

Kinaga ubaga wataalamu hao wawataka wazazi na walezi kuwa walinzi wa kwanza wa watoto wao dhidi ya matumizi mabaya ya vifaa vya kimtandao na huduma za mawasilino ili kuwa na jamii inayotambua wajibu na kuthamini maadili.

Wataalamu hao wanatoa wito huo wakati wa elimu kwa umma kuhusu usalama na matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano iliyofanyika hivi karibuni na kuhudhuriwa na wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Dk. Dawson Msongaleli, anasema wazazi na walezi wana jukumu la kwanza kuhakikisha aina ya maudhui ambayo watoto wanaangalia, kusoma au kusikiliza, hivyo kujihakikishia udhibiti wa maudhui yasiyofaa.

Msongaleli anasema siyo sahihi kumwachia mtoto wako simu apekue na kuangalia kila aina ya maudhui, lazima kuwe na udhibiti wa kifaa hizo.

Ofisa huyo wa polisi anaikosoa jamii inayojisahau kwa kudhani kuwa inakwenda na wakati kwa kuwaruhusu watoto kuwa na uhuru uliopitiliza na kupuuza kuwa ina wajibu wa kuhakikisha mienendo ya watoto wao kuanzia tabia na makuzi inawekewa mipaka ili kuwa na kizazi kijacho chenye nidhamu na viongozi bora.

> **Akaja na angalizo kuwa ni wazazi na walezi wachache wana ufahamu na namna hizo za udhibiti kwa watoto wao kutumia vifaa hivyo.**

Kaimu Mkurugenzi wa Usalama wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Stephen Wangwe anasema elimu inahitajika kwa jamii kutambua namna bora ya matumizi ya huduma za mawasiliano.

Wangwe anasema kuna namna ya kudhibiti maudhui mtandaoni na kwenye vifaa vya mawasiliano, ikiwamo simu janja na kompyuta kwa kuzingatia umri na rika kwa watumiaji.

Akaja na angalizo kuwa ni wazazi na walezi wachache wana ufahamu na namna hizo za udhibiti kwa watoto wao kutumia vifaa hivyo.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa OUT, Profesa George Oreku, anawaomba kuendelea kutoa elimu hiyo kwa jamii kwa kuwa bado kuna changamoto nyingi za matumizi mabaya ya huduma za mawasiliano nchini.

Kwa kuwa wataalamu hao wameliona hilo, kama jamii tuna kila sababu kuwadhibiti watoto wetu kutumia simu na vifaa vingine vya kielektroniki na kuwakuza katika maadili mema ili kupata raia bora.

Tukumbuke hao ndiyo Watanzania wa kizazi cha leo watakaokirithisha na kukiendeleza kijacho hivyo kuifikia Tanzania endelevu, muda bado upo hatujachelewa kila mmoja atimize wajibu.

## NEMC yatahadharisha tishio la tsumani watu wanaovamia fukwe

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetahadharisha watu wanaojenga kwenye fukwe za bahari bila kuwa na cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA).

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Utafiti wa Mazingira wa NEMC, Rose Mtui, wakati akifungua mkutano wa kimataifa kuhusu namna ya kuratibu mabadiliko ya fukwe katika nchi za ukanda wa magharibi mwa Bahari ya Hindi.

Alisema fukwe zimekuwa zikipata madhara ya mmomonyoko kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zinazotokana na shughuli za binadamu ingawa wanakatazwa na sheria.

"Kuna sheria ya mazingira inayokataza kujenga majengo ya kudumu kwenye fukwe hasa ndani ya mita 60 kwa hiyo haya mafunzo yatatoa mwanga kwa watu wanaofanyakazi ya kupanga hasa watu wa ardhi wanapotoa vibali wafuate sheria," alisema Rose ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka.

Alisema ingawa NEMC imekuwa ikifanya operesheni za mara mara na kuwaondoa watu wanaojenga majengo ya kudumu kwenye fukwe, hali hiyo imekuwa ikijirudia mara kwa mara hasa mkoani Dar es Salaam.

"Kuna watu wanapata vibali kwenye taasisi zingine kabla ya kupata kibali cha EIA kutoka NEMC na tumekuwa tukifanya ufuatiliaji kwa wale tunaowapa vibali na tukiona amekiuka maelekezo ya kibali kuna hatua tumekuwa tukizichukua," alisema.

Mkuu wa Idara ya Sayansi ya Uvuvi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Siajali Pamba, alisema kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, fukwe nyingi zimekuwa zikimomonyoka na kuhatarisha mali na miundombinu inayotegemewa kwenye uchumi wa buluu.

Alisema mmomonyoko wa fukwe huchukua muda mrefu kutokea lakini kutofanya tathmini na kuziangalia mara kwa mara kumekuwa kukisababisha athari kubwa kwenye fukwe hizo.

Alisema kongamano hilo linaunganisha nchi tatu katika ukanda wa bahari ya Hindi ili nchi hizo zote zizungumze lugha moja kuhusu wajibu wa kila mmoja na kupeana uzoefu wa namna bora ya kusimamia fukwe zisiharibiwe.

"Tunapoelekea kwenye uchumi wa buluu ambapo hoteli nyingi za kitalii zitajengwa sasa bila kuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia fukwe zetu tunaweza kujikuta tunahatarisha miundombinu hii ambayo itasaidia kwenye kutekeleza maono ya uchumi wa buluu," alisema.

"Lengo kubwa la kongamano hili ni kuamsha chachu ya watu wa mipango wasisahau sana eneo la bahari hasa kwenye fukwe waone kwamba ni sehemu yao ya kila siku ya kuangalia na kupangilia kwasababu siku hizi kila mtu anafanya anavyotaka," alisema.

Arthu Tuda, kutoka taasisi inayosimamia Sayansi ya Bahari ya WIOMSA, alisema fukwe za bahari zimekuwa zikibadilika kila wakati kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na shughuli za binadamu.

"Kuna umuhimu tukazingatia matumizi bora ya fukwe zetu ambazo zimekuwa zikikabiliwa na changamoto za mara kwa mara kama mawimbi makubwa kutoka baharini wakati mwingine tunasikia Tsunani na bahari ina mambo mengi sana kwa hiyo tunapofanya shughuli za kiuchumi tuzingatie usalama wa fukwe," alisema.




Waziri |Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Mafunzo Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) alipotembelea banda lao wakati wa maadhimisho ya miaka 20 ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wafa maji wakiogelea baharini

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Tulieni, Manispaa ya Lindi mkoani hapa, Mahamudu Ally (12) na Hussin Hassan (8), wamefariki kwa kuzama maji baada ya kuwashinda nguvu wakati wanaogelea katika mkondo wa Kiduni, Bahari ya Hindi.

Taarifa zilizothibitishwa na wazazi wa watoto hao pamoja na mamlaka husika za serikali, zinaeleza kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 26, mwaka huu.

Hassan Ally na Hamisi Hassan, wazazi wa watoto hao, wakizungumza na mwandishi wa habari hii kwa nyakati tafauti, walisema siku hiyo vijana wao waliondoka wakiwa na wenzao (12) kwenda mkondo wa Kiduni kuogelea na hawakurejea nyumbani.

Walisema kitendo cha kutorejea nyumbani kwa watoto hao, kuliwapa mshangao uliowafanya kuwatafuta wenzao waliokuwa nao ili kupata taarifa za wenzao nini kilichowapata hata wasirudi na kuelezwa kuwa waliwaacha wakiwa wanaogelea.

"Wale vijana baada ya kuwauliza walisema wenzao wamewaacha wakiendelea kuogelea kwa kutumia gubi la mnazi," alisema mmoja wa wazazi hao.

Kutokana na maelezo hayo na watoto wao kutokuwa na tabia ya kuchelewa kurejea nyumbani, walipatwa na hofu na kutoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya mtaa na kazi ya kuwatafuta ikaanza na kufanikiwa kuikuta miili yao ikiwa inaelea baharini.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kiduni, Abbas Ally, alisema katika msafara wao walikuwa watoto (12) walitumia nafasi ya kwenda pwani kuogelea kutokana na kueleza kutokuwa na masomo ili kupisha mtihani kwa wanafunzi wa darasa la nne.

> **"Baada ya kupata taarifa za kutorejea nyumbani kwa watoto hao, kazi ya kuwatafuta ikaanza na kufanikiwa kuwapata kwa nyakati tafauti," alisema Ally.**

"Baada ya kupata taarifa za kutorejea nyumbani kwa watoto hao, kazi ya kuwatafuta ikaanza na kufanikiwa kuwapata kwa nyakati tafauti," alisema Ally.


Aidha, kiongozi huyo alisema mwili wa Mahamudu ulipatikana siku hiyo hiyo usiku na Hussein siku ya pili saa 3:30 asubuhi na kufanyiwa uchunguzi na mganga wa Kituo cha Afya Mnazi Mmoja, Dk. Rajabu Shegila.

Dk. Shegila akithibitisha kutokea kwa vifo vya watoto hao, alisema sababu ya vifo hivyo kutokana na kukosa hewa ya oksijeni baada ya kuzama ndani ya maji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) John Imori, alikiri kutokea kwa vifo vya wanafunzi hao na kuwataka wazazi kuwa makini na vijana wao, ikiwamo kuwazuia kupendelea kwenda baharini kuogelea kwa kuwa ni hatari kwa usalama wa maisha yao.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



HABARI KITAIFA

# ACT yaomba kuungwa mkono

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WANANCHI wa Wilaya ya Tunduru wameshauriwa kubadilika na kukiunga mkono chama cha ACT - Wazalendo kwa kukichagua katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Katibu Mkuu wa ACT - Wazalendo, Addo Shaibu, alisema hayo kwenye mkutano wa hadhara wa chama hicho wa kuwashukuru wananchi kwa kuwaunga mkono kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Shaibu aliwashukuru wananchi kwa kuwaunga mkono katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 katika wilaya hiyo kwenye majimbo ya Tunduru Kusini na Tunduru Kaskazini. Katika uchaguzi huo, chama hicho kilimsimamisha Mtutura Abdalah Mtutura, Tunduru Kusini na Tunduru Kaskazini, Shaibu ambao alisema walishinda ingawa hawakutangazwa.

Alisema kutokana na hali hiyo, yuko tayari kuendelea kupambana ili wakipewa ridhaa ya wananchi wawatumikie na kuweka mchango wao kwa jamii yao.

Mwenyekiti wa Selous, Abdalah Mtalika, alisema mkutano huo unahitimisha ziara iliyofanywa na chama hicho kwa ajili ya kuwashukuru wananchi waliokiunga mkono kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Aidha, Mtalika alidai kuwa viongozi wa Tunduru wanadhulumu wananchi mazao kwa kununua korosho zao kwa mfumo holela maarufu kwa jina la Kangomba ingawa hakuwataja majina hadharani.

Katibu wa Mkoa wa Kichama wa Selous, Mtutura, alisema uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 aliporwa na wateule ambao huapa kuilinda katiba.

Akizungumzia kilichomtoa CCM, alisema ni msimamo wake wa kukataa stakabadhi ya mazao ghalani na msimamo wake wa kuwatetea wananchi juu ya matukio ya tembo.

Mtutura alisema pamoja na upungufu uliomo ndani ya katiba ya Tanzania, yamo mambo mazuri na akanukuu ibara namba 14 inayozungumzia ulinzi na usalama wa wananchi na ibara namba nane inayozungumzia haki za wananchi.

Alisema mauaji yanayosababishwa na tembo ni mengi kwa wananchi, akitolea mfano vijiji vya Mtonya watu wanne, Kazamoyo (watatu), Marumba na maeneo mengine watu wameuawa na tembo lakini hakuna tembo aliyeuawa.



Hata hivyo, alisema mwaka huu aliuawa tembo mmoja baada ya kutaka kumjeruhi ofisa wa idara ya maliasili.

Kuhusu bei ya korosho katika msimu wa mwaka 2023/24, alisema wananchi hawajaridhika nayo, hivyo amepanga utaratibu wa kuijulisha serikali kama hawatasikia matokeo yake watayaona wenye uchaguzi mwaka 2024 na 2025.

Naye Diwani wa Mchoteka, Jimbo la Tunduru Kusini, Seif Dauda, alisema katika wilaya ya Tunduru, kutokana na kadhia ya mifugo, hakuna aliye salama.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo Jimbo la Tunduru Kaskazini, Mawila Said, alisema kumekuwa na matukio ya mauaji ya madereva wa bodaboda huku serikali ikiwa imekaa kimya na kuhoji kama serikali ingekaa kimya kama askari polisi angeuawa.



Waziri wa Madini wa Malawi, Monica Chang'anamuno (kushoto), akikabidhiwa tuzo ya juu ya kuchangia pato la serikali na Ofisa Mawasiliano wa Twiga Minerals Corporation, Abella Mutiganzi (katikati), kwa niaba ya kampuni katika hafla ya usiku wa madini iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Waziri wa Madini, Antony Mavunde. Twiga pia ilishinda tuzo maalum ya umiliki wa leseni ya uchimbaji wa madini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yataka wajasiriamali wachangamkie nembo

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI wameshauriwa kutumia fursa ya mpango wa serikali wa kukuza viwanda vidogo na vya kati kujitokeza kwa wingi kupatiwa nembo ya ubora kwa gharama za serikali.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa itawawezesha kuongeza ubora wa bidhaa zao, kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi na kuzalisha bidhaa ambazo zina uwezo wa kushindana katika soko la Tanzania na Afrika Mashariki.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Uthibiti Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Mashariki, Francis Moshi, kwenye maonesho ya kwanza ya Wakala wa Usajili wa Biashara (BRELA) na wadau wake yaliyofanyika Viwanja vya Mlimani City, Dar es Salaam.

Alisema wameshiriki maonesho hayo ili kueleza huduma ambazo wanatoa, kwani wao ndiyo wanaohusika wa kusajili na kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa nchini na zile zinazotoka nje zinakidhi vigezo vyote vya ubora.

Moshi alisema TBS kwa kushirikiana na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), wameanzisha mpango wa kuhakikisha wajasiriamali wanazalisha bidhaa ambazo zina ubora ili ziweze kushindana sokoni.

Kwa sababu hiyo, Moshi alisema wana jukumu kubwa la kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa na wajasiriamali nazo zinakidhi ubora.

Alisema mjasiriamali yeyote ambaye anazalisha bidhaa anatakiwa kupata nembo ya ubora ya TBS.

Kwa mujibu wa Moshi, mjasiriamali anatakiwa kwanza apitie SIDO na kupatiwa mafunzo mbalimbali yanayohusu bidhaa anazozalisha na SIDO watamfanyia ukaguzi wa maeneo yake.

Alisema baada ya ukaguzi watamwelimisha namna bora ya kuzalisha bidhaa zake na kisha ataandikiwa barua ya utambulisho kwenda TBS.

"TBS tukishapata barua ya huyo mjasiriamali, tutampatia huduma na nembo ya ubora ya TBS bure kabisa. Atakaa nayo miaka mitatu bila kulipia gharama yoyote na kuanzia mwaka wa nne kadri itakavyoonekana ataanza kulipa asilimia 25 ya ile ada ambayo alitakiwa ailipe," alisema.

Naye mjasiriamali, Werema Julius ambaye alishiriki maonesho hayo alisema alifika banda la TBS ili kufahamu namna gani biashara yake ya chakula inaweza kuthibitishwa ili kuwezesha wateja wake kupata kilicho bora na kinachoaminiwa na serikali.

# Katibu wa ushirika anusurika kifungo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, imemuhukumu Katibu wa Chama cha Msingi na Ushirika cha Umoja AMCOS, Rahim Tewele (40), kulipa Sh. milioni mbili kutumikia kifungo cha miaka saba gerezani baada ya kukutwa na hatia ya uhujumu uchumi.

Hata hivyo, Tewele alifanikiwa kulipa kiasi hicho cha fedha, hivyo kunusurika kwenda jela kutumikia adhabu hiyo.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Christopher Makwaya baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka kutokana na kosa lililomkabili.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Hakimu Makwaya alimpa mshtakiwa nafasi ya kujitetea ili mahakama isimpe adhabu kali na kuiomba imwonee huruma kwa madai anayo familia inayomtegemea wakiwamo mke, watoto wanne na wazazi wawili.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Makwaya alimuuliza mwanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, Salum Bhoke, kama ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hakuna huku akiiomba mahakama kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Akitoa hukumu hiyo katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 17/2023 kupitia kifungu cha 342 cha Sheria ya Kanuni ya adhabu sura 16 marejeo ya mwaka 2019, Hakimu akamhukumu mshtakiwa Tewele kulipa faini ya Sh. milioni na akishindwa akatumikie kifungo cha miaka saba gerezani.

Mshtakiwa Tewele alilipa faini aliyotozwa na mahakama, hivyo kunusurika kupelekwa gerezani kutumikia kifungo.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na mwanasheria wa TAKUKURU Bhoke kuwa mshtakiwa Tewele akiwa Katibu wa UMOJA AMCO'S Mbwemkuru, alitumia madaraka vibaya ikiwamo kughushi nyaraka za malipo zinazoonyesha watu watatu walipeleka kwenye chama hicho korosho msimu wa mauzo 2019/20.

Bhoke alidai kuwa kutokana na hatua hiyo, mshtakiwa akiwa anatambua anachokifanya ni kosa, aliwasilisha majina hayo kwa ofisa ushirika wilaya ya Liwale kwa ajili ya malipo na kujipatia Sh.16,575,776,837/43 kwa njia za uongo.



## Zimamoto yasisitiza ukaguzi ramani makazi

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji, limesisitiza umuhimu wa kufanyika ukaguzi wa ramani za ujenzi wa makazi na nyumba za biashara ili kudhibiti ujenzi holela na kurahisisha uokoaji wa watu na mali zao majanga yanapotokea.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Tanga, Leonard Mponeza, aliyasema hayo jana wakati akitoa elimu ya ukaguzi, kinga na tahadhari ya majanga ya moto kwenye kikao kazi kinachohusisha wadau wa kada mbalimbali.

Kikao hicho kiliwahusisha wafanyabiashara, Halmashauri, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mji, maofisa watendaji kata na wadau wa maendeleo Wilaya ya Muheza.

Alisema madhumuni ya kikao hicho ni kutoa elimu ya kinga na tahadhari za majanga ya moto na kulipia tozo kwa jeshi hilo, ikiwa ni pamoja na usomaji wa ramani za majengo na kutoa ushauri juu ya usalama wa maisha ya watu na mali zao katika majengo hayo.

Mkaguzi Msaidizi wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Tanga, Hussein Mahamdu Hussein, alisema ukaguzi na kulipia tozo ni takwa la kisheria.

Alisema maeneo yote ya biashara, makazi na taasisi ni lazima yakaguliwe na kulipia tozo hizo.

Hussein alisema kabla ya kuanza ujenzi wa makazi na sehemu za biashara ni lazima ramani za majengo zipitiwe na maofisa wa jeshi hilo ili kutoa ushauri wa jinsi ya kukabiliana na majanga ya moto na namna ya kujiokoa wakati wa dharura.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Muheza, Johari Mtango, aliwasihi wafanyabiashara kuacha visingizio kwa kulipia tozo na kukabidhi ramani za majengo kwa maofisa wa Zimamoto ili kuijenga Muheza mpya na ya kisasa.

Mbunge mstaafu wa Muheza, Hebert Mtangi, aliutaka uongozi wa wafanyabiashara hao kuhakikisha wanatoa ushirikiano wakati wa ukaguzi wa ramani za majengo na ulipiaji wa tozo hizo.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji wa Muheza, Seif Twenye, aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa halmashauri hiyo inatambua umuhimu wa huduma za Zimamoto na Uokoaji.

Alisema wafanyabiashara wanapaswa kuishukuru serikali kwa kusogeza huduma kwa kuanza kufungua ofisi za jeshi hilo, na kuahidi gari la zimamoto liko mbioni kununuliwa.

# Wapendekeza mjadala mmomonyoko wa maadili

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKAZI wa Kijiji cha Lole, Moshi mkoani Kilimanjaro, wamependekeza kuitishwa kwa mjadala wa kitaifa kuhusu kuporomoka kwa maadili ya Mtanzania.

Mjadala huo, pamoja na mambo mengine ni kujadili baba kuzaa na mwanawe, kwa mfano na njia gani inaweza kutumika kurejesha utaratibu wa zamani wa jamii kumwona mtoto wa mwenzake ni wake.

Aidha, wametaka serikali na wadau wanaoendesha mapambano ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kuandaa mpango mahususi wa utoaji elimu ili kukabiliana na kundi la vijana wanaowazalisha wasichana na kuwaacha.

Akizungumza jana, mkazi wa kijiji hicho, Heriamin Kimei, alisema kwa namna hali ya ukatili ilipofikia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Maundi Maalum, inapaswa kuliangalia upya suala la kukosekana kwa matunzo na watoto wasiolelewa na wazazi wawili, huku idadi ya wanawake wanaoongoza kaya ikiongezeka.

Wananchi hao walipendekeza mambo hayo wakati wa mkutano wa utoaji elimu ulioendeshwa na Shirika la Kiraia la KWIECO, linalofadhiliwa wa Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), kupitia mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto.

"Kuna haja ya kuwa na mjadala mpana wa kitaifa, kufanya tathmini na kujadili tunaweza kurejesha utaratibu huo ili kukabili mmomonyoko wa maadili unaoendelea. Mambo sasa hivi yanaenda ndivyo sivyo, tusipofanya hivi tunaliyumbisha taifa na watoto au vijana hawana tena kitu cha kuiga kutoka kwetu," alisisitiza Kimei.

Mkazi mwingine, George Mamkwe, alisema: "Tunataka kuipa tena jamii nguvu ya kumwadhibu mtoto anayekwenda kinyume. Wanachofanya vijana wengi hivi sasa, hawaoni kama ni ukatili. Hawatoi matunzo na wala hawana mpango wa kuhudumia hao watoto. Watoto wasio na wazazi wawili wanaongezeka na idadi ya wanawake wanaoongoza kaya inaongezeka."

Naye Redfan Mringo, aliwanyooshea kidole wakazi wa kijiji hicho wanaotengeneza mazingira ya rushwa kwa askari polisi ili kupindisha ufikiwaji wa haki baada ya kutuhumiwa au kukamatwa na kesi za ukatili wa kijinsia.

"Wengine wanaua kesi kwa kupeana masale (majani ya mila ya Wachaga). Hii hapana kwa kweli. Masale yameathiri sana haki na watu wengi wamekosa haki na hilo jani haliangalii nani ameathirika," alisema Vivian Shao.

Akitoa elimu kwa wakazi wa kijiji hicho, Mratibu wa Mradi wa Jitihada za Jamii katika Kuzuia na Kutoa Taarifa dhidi ya Wanawake na Watoto, Veronica Ollomi, aliwasihi wananchi hao kuchukua hatua.

"Hebu tuchukue hatua. Kama baba una wajibu gani katika familia? Tusiachie kinamama peke yao katika uangalizi wa watoto. Biblia inasema mtoto akiharibika, mwana mpumbavu ni mzigo kwa mamaye. Tutimize wajibu wetu, wewe kama baba wa familia umekaaje kwenye nafasi yako? "Mchungaji anaweza akahubiri kanisani, akatumia na Biblia lakini hafiki kila mahali, ninyi mkiwepo kanisani, ataongea na ninyi lakini kwenye ngazi ya kaya kule hajui, labda mtu aende akamwambie.

"Tunazo kesi nyingi za watoto wa kiume kulawitiwa, jamani Mchungaji! Kama ni kufunga tufunge kwa sala ili kuwanusuru watoto wa kiume. Kesi za watoto kulawitiwa na kubakwa zimekuwa ni tishio na sio kwamba ni vitu vya kuficha, lakini tu ni kwa vile jamii tumeamua kuvifumbia macho, kukaa na kuendelea na maisha yetu," alisema.



Maofisa wa polisi wakiwa wamebeba sanduku lenye mwili wa marehemu Zelothe Stephen aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM mkoani Arusha, katika maziko yaliyofanyika jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# TCB yataka ufumbuzi changamoto kahawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TIJA katika uzalishaji wa kahawa nchini, inatishiwa na mambo tisa yanayosubiri mkono wa serikali na juhudi za wadau walioko kwenye mnyororo wa thamani, kupata ufumbuzi wa kudumu wa namna bora ya kuinua uzalishaji wa zao hilo la kimkakati, linalotegemea mauzo ya nje kwa asilimia 93.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Prof. Auleria Kamuzora, licha ya kuonekana kiwango cha uzalishaji wa kahawa kwa miaka miwili iliyopita ukipanda, ujio wa kahawa inayozalishwa bila kutumia kemikali, unafikirisha na unahitaji mdajala mpana wa kitaifa, kwa kuwa ina bei kubwa kuliko kahawa inayozalishwa kwa kemikali hivi sasa.

Prof. Kamuzora alikuwa akizungumza na wadau wa zao hilo mwishoni mwa wiki katika Mji wa Moshi, Kilimanjaro, wakati wa kufunga Tamasha la Kahawa Festival la Mwaka 2023.

"Kwa hiyo hilo la 'organic coffee' (kahawa isiyotumia kemikali) tunaendelea kulifanyia kazi tuone ni vipi tunaweza kubalance (kuweka usawa) uzalishaji wa kahawa ambayo tunaita ni sustainable agriculture (kilimo endelevu). Je, serikali yetu inakuwa imejipangaje?

"Tuna magonjwa yanayoathiri kahawa. Haya magonjwa bodi inatakiwa kuyafanyia kazi na bado inaendelea kupambana na tatizo hili," alisema.

Prof. Kamuzora alitaja tatizo lingine linaloikabili sekta ya kahawa ni kukosekana kwa pembejeo za uhakika, kwa kuwa dunia imebadilika na mlaji anajiuliza ni pembejeo gani imetumika ili anunue kahawa yako.

Pia, liko tatizo la miti mingi ya kahawa nchini kuonekana kuwa na umri mkubwa na hivyo kupunguza tija ya uzalishaji.

Katika ripoti yake, Prof. Kamuzora, ameeleza kuwa kushuka kwa rutuba ya udongo katika baadhi ya mikoa ambayo inazalisha kahawa kama Kilimanjaro, baadhi ya maeneo udongo unachangia kupunguza thamani.

"Mabadiliko ya tabianchi, nayo yanaathiri sekta ya uzalishaji kahawa lakini tukiweka juhudi zaidi tunaweza kuhimili na kutatua tatizo hili.

"Na vilevile kuna tatizo la vijana wengi kutoingia kwenye mnyororo wa thamani wa zao la kahawa. Vijana wengi wanaoenda kutafuta kazi ambazo haziwafanyi waende shambani," alisema.

Mnyororo wa thamani wa kahawa una mambo mengi, wanaweza wakaingia kwenye kuuza, kununua, kukaanga na wanaweza wakawa na coffee shops (maduka ya kahawa) wakafanya kazi. Lakini tunalo pia tatizo la kutoongezeka kwa tija," aliongeza.


Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Francis Kajiru, alisema tamasha hilo la siku tatu lililoanza kufanyika Oktoba 27 hadi 29 mwaka huu, ni mahusus kwa wadau wote kusherehekea mafanikio yao, kwa kuwa sekta ya kahawa imeanza kukua na kuonyesha mafanikio tena.

"Tutazitumia changamoto zilizoko kufanya vizuri zaidi, kwa sababu ziko changamoto ambazo bado hazijatatuliwa na kutekelezeka sawa sawa ili kupata suluhisho lake," alisema Kajiru.

Awali, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau wa Kahawa nchini, Denis Mahulu, akizungumza katika tamasha hilo alisema: "Tuna mpango wa kuongeza unywaji wa kahawa katika eneo la vyuo vikuu na kuanzisha mobile coffee shops (maduka yanayotembea ya kahawa) ambavyo yatawezesha kuongeza unywaji wa kahawa."

Kiwango cha unywaji wa kahawa nchini, kimeongezeka kutoka asilimia 5 hadi kufikia asilimia 7, huku serikali ikiweka wazi mkakati wake ni kupandisha zaidi kiwango hicho mpaka asilimia 15, ifikapo mwaka 2025/2026.

Aidha, wastani wa uzalishaji wa zao hilo la kimkakati nchini, kwa sasa umepanda kutoka tani 50,000 hadi kufikia tani 82,000 mwaka huu.



# Wananchi walivyofichua wizi mifuko 600 saruji

**Na Vitus Audax**

WANANCHI wa Kijiji cha Karukekere, Bunda mkoani Mara wamefichua wizi wa zaidi ya mifuko 600 ya saruji yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 23 inayodaiwa kuibwa katika mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mara wenye thamani ya Sh. bilioni nne.

Wananchi hao wamesema wamebaini saruji hiyo ambayo ilikuwa ikifikishwa nyumbani kwa Nyandago Magessa majira ya jioni na usiku ikisombwa na magari yaliyotajwa kuwa ya serikali, hivyo kuamua kutoa taarifa kwa vyombo vya dola.

"Tuliona gari la kwanza linaleta mzigo ukapakuliwa na kuingizwa ndani ya nyumba ndipo wananchi tukaanza kupata hofu kwamba hii saruji kwa utaratibu inaletwa na serikali mbona sasa inaletwa nyumbani kwa mtu, ikabidi kutoa taarifa," alisema Joshua Omindendeya, mkazi wa kijiji cha Karukekere.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Daniel Peter, alisema baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wasamaria wema, walihisi saruji hiyo kuwa ya wizi ikitoka katika mradi huo wa shule ulioko kilometa 15 kutoka kijijini. Hatua hiyo ilimfanya afikishe taarifa hiyo kwa mkuu wa wilaya aliyefanikisha ukamataji wake.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vicent Naano, aliagiza kukamatwa kwa mmiliki wa nyumba hiyo, Magessa, huku akitoa onyo kwa mtu yeyote atakayejihusisha na wizi katika miradi ya serikali.


"Aliyekamatwa na ngozi ndiye mwizi na wewe utatusaidia katika uchunguzi. Haiwezekani saruji ya serikali ikutwe katika nyumba yako bila wewe kuwa na taarifa na saruji hii inatumika katika miradi ya serikali pekee halafu ikutwe kwenye nyumba ya mtu binafsi," alisema Dk. Naano.

Mkuu huyo wa wilaya aliongeza kuwa saruji hiyo inayonunuliwa na serikali kwa gharama ya Sh.24,000 ilikuwa ikiuzwa na watu hao kwa Sh. 21,000 hali ambayo ilitiliwa shaka upatikanaji wake.

Akizungumza kabla ya kukamatwa, Magessa alikana kuitambua na kusema ililetwa na mdogo wake ambaye aliomba chumba hicho kwa ajili ya matumizi yake ambayo hakuyataja.

"Aliniuliza kuwa chumba chako kiko wazi nikamweleza kuwa kiko wazi akaniuliza unaweza kunikodishia kwa shilingi ngapi, nikamwuliza unataka kufanyia nini hakunieleza," alijitetea Magessa.

Mradi huo wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkoa wa Mara unaotekelezwa wilayani Bunda, unatarajia kugharimu zaidi ya Sh. bilioni nne huku serikali ikiwa tayari imetoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya utekelezaji wake.




Meneja wa Airtel Kanda ya Ziwa, Brighton Majalwa (kushoto) na Meneja Biashara wa Airtel Shinyanga, George Michael, wakimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 50 mshindi wa promosheni ya Upige Mwingi na Airtel mkazi wa Manispaa ya Shinyanga, Renatus Mashauri (katikati), katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wazee 1,480 wapewa bima iliyoboreshwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZEE 1,482 wanaoishi katika mazingira magumu Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamewezeshwa Bima ya Afya ya CHF iliyoboreshwa ili kupata matibabu bure kwa gharama nafuu zikiwa na thamani ya Sh. milioni 7.440.

Katibu wa Baraza la Wazee Taifa, Mzee Anderson Lymo, aliyabainisha hayo juzi kwenye kikoa cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 na kusema sasa wanaendelea kupata matibabu bure na hakuna malalamiko dhidi yao.

Alisema wazee 1,482 wamepatiwa bima hiyo na kwamba kati ya hizo 1,200 za Sh. milioni sita zilitolewa na Manispaa ya Kahama, 70 na Kanisa la Mito ya Baraka kwa Sh. 360,000, Maritus Foundation bima 92 kwa Sh. 480,000 na mdau wa afya Emmanuel Kidenya bima 120 kwa Sh.600,000.

Lymo alisema manispaa hiyo ina wazee 6,692 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kati ya hao, wazee 5,210 wana bima ya afya ya CHF iliyowaboreshwa inayowasaidia kupata matibabu katika vituo vya afya, zahanati na hospitali za wilaya na mikoa na baadhi yao wanabima ya NHIF.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ufuatiliaji ya Baraza la Wazee, Laurent Nkwabi, alisema licha ya halmashauri kuwatengea fedha kila mwaka za kukata bima za wazee na kuhuisha zilitumika kwa mwaka husika, bado kuna wadau wa afya wamekuwa wakijitoa na kuwakatia wazee bima zinazowawezesha kupata matibabu bure.

**Lymo alisema manispaa hiyo ina wazee 6,692 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kati ya hao, wazee 5,210 wana bima ya afya ya CHF**

# Matumizi mabaya pempasi yageuka tishio

**Na Restuta Damian**, BUKOBA

BAADHI ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wameiomba serikali kupitia maofisa mazingira kutilia mkazo udhibiti wa utupaji ovyo wa taka aina ya pempasi ambao umekithiri katika makazi ya watu na kuhatarisha afya zao.

Wakazi hao walitoa kero hiyo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe iliyotembelea baadhi ya mitaa na kubaini uchafuzi huo katika makazi ya watu pamoja na barabara.

Walisema juzi kuwa taka hizo zimekuwa zikitupwa kwa wingi nyakati za usiku hali inayosababisha kushindwa kuwabaini watu hao huku wakiwatuhumu wanawake wenye watoto wadogo kuwa chanzo.

Mkazi wa Kata ya Rwamishenye Manispaa ya Bukoba, Happiness Julius, alisema si vyema kutupa ovyo pempasi na kushauri kutumika kwa utaratibu mzuri wa kuzitunza katika sehemu moja kisha kupelekwa katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

Kadhalika, alisema baadhi ya wanawake wenye utaratibu wa kwenda kufulia maeneo ya mtoni, wamekuwa wakitupa pia taulo za kike hali ambayo imekuwa ikichafua vyanzo vya maji.

Mfanya usafi wa mazingira Manispaa ya Bukoba, Kokwendela Alfred, alisema utupwaji wa taka hizo umekuwa kero katika kazi zao na kwamba wamekuwa wakikutana na taka aina mbalimbli lakini zinazofikirisha ni zile zenye aibu zaidi kama taulo za kike na pempasi.

"Anapita mtu anatupa uchafu ulipomaliza kusafisha na ukimwambia atajibu wewe fanya si umeajiriwa na manispaa kufanya usafi? Toa wewe watakulipa mshahara kwani wasipoutupa uchafu utafanya kazi gani?" alisema Alfred. Ofisa Afya na Mazingira Mkoa wa Kagera, Zabron Segeru, alisema sheria ziko wazi juu ya uchafuzi wa aina yoyote, hivyo kuwataka wananchi wenyewe kuwa walinzi wa utekelezaji wa sheria na kanuni hizo ili kudhibiti uchafuzi wa aina yoyote wa mazingira.

Alisema ni vizuri zaidi jamii kuzingatia kanuni bora za afya na si utupaji ovyo wa taka kwa kuwa uchafu huo unaingia katika vyanzo mbalimbali vya maji ambavyo binadamu atatumia kisha kusababisha madhara ya kiafya.



Ukurasa 12

Jokate anapohimiza mapinduzi 'kiwanda' kuzalisha raia bora



Ukurasa 13

Wadau wanapoandaa 'pepo' ya wabunifu, ila wasichana wakikosekana uwanjani



**Ni miaka 50 ya mapinduzi ya simu duniani zikianzia Amerika**

Ukurasa 14

Nipashe TESA

Jumanne Oktoba 31, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMU

NA MARCO MADUHU, KISHAPU

# Rais Samia alivyowaokoa mamia wasiliwe na wanyama hatari

VIJIJI kukosa shule, lakini kukosekana mabweni na wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shuleni kunazusha balaa kubwa ikiwamo watoto kujeruhiwa hata kuuliwa na wanyama pori.

Simulizi ya wanafunzi wa Kijiji cha Winenekeja wilayani Kishapu, Mkoa wa Shinyanga linatosha kufahamisha umma kuwa uzipojenga shule karibu na wanakijiji utatishia maisha ya watoto ambao watapata mimba utotoni, kunyanyaswa kingono ikiwamo kubakwa na kulawitiwa lakini kuuawa na wanyama wakali.

Wanafunzi wanapitia magumu kama wanavyoeleza watoto hawa wa Winenekeja kuwa wakati wanatoka shuleni wanafunzi walikimbizwa na fisi, wanaokula kila kitu mpaka binadamu.



Shule mpya ya msingi katika Kijiji cha Winenekeja itakayowaondolea adha wanafunzi kusoma umbali mrefu pia kuhatarisha maisha yao. **PICHA:MARCO MADUHU**

Japo walinusurika kifo baada ya wananchi kuwaokoa, fisi mmoja kati ya wanyama hao aliyekuwa na hasira alikimbia na begi la vitabu na madaftari la mmoja wa watoto hao aliyemvamia.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Winenekeja, Jonas Nkondu, anasema kukosekana kwa shule kijijini hapo si hofu kwa wanafunzi, hata kwa wazazi na walezi kwa sababu maisha yao yanakuwa hatarini kutokana na kutembea zaidi ya kilometa nane kuifikia Shule ya Msingi Igaga iliyoko kata jirani.

Anazungumza hayo hivi karibuni wakati kijiji hicho kinasherehekea kujengwa na kuzinduliwa shule ya mpya ya msingi ambayo ni mkombozi kwa watoto wadogo na wakubwa kutokana na kunusuru maisha yao lakini pia kupunguza uchovu unaotokana na kutembea kilometa nyingi na kurudi nyumbani kila siku kwa miaka saba ya elimu ya msingi.

Nkondu anasema Wilaya ya Kishapu inakabiliwa na idadi kubwa ya fisi ambao wamekuwa wakizagaa ovyo hasa majira ya alfajiri pamoja na jioni, hivyo kukutana na watoto wakati wakijihimu kuwahi shuleni na kurudi nyumbani.

"Niwakumbushe mwaka jana watoto walikimbizwa na fisi wakati wakitoka shule lakini tunashukuru hakuna alijeruhiwa sababu wananchi waliwaokoa, japo fisi aliondoka na mfuko wa vitabu na daftari."

Anasema katika kuwalinda watoto wao na fisi hao, waliitisha Mkutano wa wanakijiji na kisha suala hilo kulikabidhi kwa jeshi la jadi sungusungu, ili kuwalinda alfajiri wanapoamka kwenda shule na jioni wakirudi nyumbani, angalau kukawepo na unafuu kiusalama.

Mzazi Maria Kulwa, anasema umbali wa shule ni tatizo watoto wao kusoma kwa amani, na kueleza kwamba licha ya kuwa katika hatari ya kushambuliwa na fisi, pia kipindi cha mvua wanapata shida na wakati mwingine inayowazuia watoto wa darasa la kwanza wasiende shule, kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya na kusababisha kukosa masomo.

"Sisi kinamama tunaumia zaidi hasa tunapoona mtoto anasoma katika mazingira ambayo siyo salama, watoto wetu wakienda shule tunajaa wasiwasi kama watarudi salama nyumbani au watadhurika muda wote tunakuwa na hofu," anasema Maria.

Diwani wa Igaga wilayani Kishapu James Kamoga, anasema moja ya kilio kikubwa cha wanakijiji cha Winenekeja ilikuwa ni shule ya msingi, na walikuwa wakilijadili suala hilo kwenye vikao vya kamati ya kata na kushurukuru kuwa ufumbuzi umepatikana na sasa shule imejengwa kijijini humo.

Aidha, anasema shule hiyo mpya ya Msingi Winenekeja ina vyumba vya madarasa 16, matundu ya vyoo 24 na itaanza kazi mwakani na ikijengwa kwa gharama ya Shilingi milioni 561.

"Tunaishukuru serikali kwa kutujengea shule hii mpya ya msingi, kilio hiki cha wananchi sasa kimepata ufumbuzi, na watoto hawatakuwa tena katika hatari ya kushambuliwa na wanyama hasa fisi," anasema Kamoga.

Anawasihi wazazi na uongozi wa kijiji kwa kushirikiana na Sungusungu, kuendelea kuimarisha ulinzi kwa wanafunzi ambao wataendelea kusoma katika Shule ya Msingi Igaga ili kumalizia masomo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, anasema ndani ya miaka miwili na nusu ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, wilaya hiyo imeshapokea bilioni 40.4 na kutekelezwa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali, ikiwamo ya elimu kwa kuboreshwa miundombinu yake na kujengwa shule mpya mbili za msingi.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Jokate anapohimiza mapinduzi ‘kiwanda’ kuzalisha raia bora

MMOMONYOKO wa maadili ni tatizo linalolikabili taifa na maeneo mengi barani Afrika, tena ukihatarisha mustakabali mwema wa kizazi cha sasa na kijacho.

Ni kwasababu uwepo wa vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili, mila, desturi na taratibu za maumbile si tu kwamba vinatishia maisha na hali ya binadamu asilia bali pia ni adui wa maendeleo yake.

Ni dhahiri shahiri kuwa hatua zinapaswa kuchukuliwa kuanzia ngazi ya familia, jamii na nchi kwa ujumla ili kunusuru watoto na mmomonyoko wa maadili unaohatarisha kila nyanja ya maisha kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Wazazi na walezi ni wadau muhimu katika mapambano haya ya kukengeuka ambayo wasichana kwa wavulana wa kizazi cha sasa wamezamishwa katika bahari ya uharibifu.

Ni ukweli kuwa hakuna namna ambayo wazazi na walezi wanaweza kujitenga na mienendo mibaya ya kitabia ya watoto na wategemezi wao kutokana na momonyoko wa maadili ya watoto unaoonekana leo hasa kuanzia ngazi ya familia.

Katika saikolojia ya makuzi ya watoto inaaminika kuwa, kila mtoto anayezaliwa ana tabia njema ila jamii anayokutana nayo ndiyo inaamua kama ataendelea kuwa mwenye tabia njema (proper behaviour) au kuwa na mbaya (improper behaviour).

Wataalamu wa akili za watoto wanaeleza kuwa mtoto anapozaliwa huwa hajui chochote na ubongo wake umetakata, hafahamu kutukana, kuiba, kudharau watu wala aina yeyote ya mienendo mibaya, kwani mtoto huzaliwa akiwa na kila kitu chema kisicho na mawaa.

Makuzi anayopata mtoto kuanzia katika familia na jamii inayomzunguka ndiyo yenye kutoa mwelekeo wa aina ya tabia na maadili kama mazuri au mabaya.

Hivyo malezi bora kuanzia ndani ya mikono ya baba na mama na walezi wengine kwenye familia yake ni muhimu sana katika kujenga tabia njema ya raia huyo mchanga.

Maandiko matakatifu yanasisitiza maelezi bora na kutumia fimbo wenye watoto wakiaswa wasiche kutumia kiboko.

Aidha, wanakumbushwa kuwa mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.



Malezi bora na utii kwa walimu pamoja wazazi huwafikisha watoto kwenye furaha kama kuhitimu masomo yao. **PICHA: MTANDAO**

> Hatuwezi kuwa na viongozi bora bila kutengenezwa, kizazi bora kinachotoka kwenye familia au kwa wazazi na walezi, hivyo jukumu hilo haliwezi kukwepeka.

Kutokana na ukweli kuwa mtoto huzaliwa akiwa na tabia njema na maadili mazuri, mlolongo huo unapaswa kuendelezwa pale anapozaliwa hadi ukuaji wake wote.

Ndiyo maana maandiko matakatifu yanasisitiza kuwa mzazi anawajibika kumlea mtoto katika njia nzuri na msingi huo utakaowekwa na mzazi au mlezi, utamsaidia mtoto kuendelea na tabia njema hiyo si tu katika utoto wake bali hata katika ujana, utu uzima na uzee wake wote.

Kwa wazazi au walezi ambao wanafahamu kuwa ni wajibu wao kusimamia mwenendo na tabia za watoto wao kuna ujumbe wa Jokate Mwegelo, huyu ni Katibu Mkuu wa UWT.

Anaeleza hayo mwishoni mwa wiki iliyopita anapozungumza na wanahabari akisisitiza suala la maadili kwa watoto akiwataka wazazi na walezi kutimiza wajibu wao usiokwepeka wa kuwalea watoto katika njia bora ili kuwa na viongozi na raia bora katika jamii.

“Wazazi wanatakiwa kushika nafasi zao za ulezi na kuongoza watoto na kuwasaidia, kipindi hiki tunaona wazazi na walezi wanawaogopa watoto kuliko watoto wanavyowaogopa wao,” anasema Jokate.

Anachoeleza Jokate ni jambo la kweli kabisa kwa vile mzazi au mlezi anageuka kuwa mtumwa wa mtoto wake.

Anafafanua kuwa ni kutokana na kuyumba kwa maadili ya watoto ndiko kumesababisha hayo lakini kukichangiwa pia na baadhi ya walezi kushindwa kubeba majukumu yao kikamilifu ya malezi na hivyo watoto kujiongoza wenyewe.

“Tumefikia hatua mbaya ambayo wazazi na walezi tunaogopa kukemea tabia mbaya wanazozoiona kwa mtoto au watoto wetu. Mathalani, mtoto anaweza kuwa mwizi, kutumia dawa ya kulevya, kujihusisha na ngono, lakini mzazi au mlezi akafumbia macho vitendo hivi na wakati mwingine kuwa mtetezi wa mtoto wake pindi anapopewa taarifa za tabia mbaya dhidi ya mtoto wake.”

Aidha, baadhi ya wazazi na walezi hawana muda kuangali maisha na mienendo ya watoto na wategemezi, hawaongei nao kujua changamoto, mipango wala shida zao na namna ya kuzitatua.

Anawakumbusha kuwa ni muhimu kuwa na muda wa kutosha wa kuongea na watoto ili wajue yale wanayayopenda, yanayowasumbua, wanayopitia na yapi yanayowatatiza.

Ni muhimu kupandikiza maadili na tabia njema kwa watoto ili wakue wakiyaishi yale waliyofunzwa na wazazi na walezi wao.

“Tukifanikiwa kujenga maadili mema katika ngazi ya familia, hata nchi itakuwa na raia wema kwani watoto ni raia pia, ambao ndiyo warithi wa wazazi ma walezi wao kwa siku zijazo,” anakumbusha Jokate.

Kwa mujibu wa maelezo yake mafanikio ya malezi mazuri katika familia yanaleta manufaa ya kupata viongozi bora katika ngazi zote, akisisitiza pia wazazi kulea watoto katika maadili mazuri ili kupata viongozi bora kwani familia ni kiwanda cha kuzalisha viongozi bora pia.

“Hatuwezi kuwa na viongozi bora bila kutengenezwa, kizazi bora kinachotoka kwenye familia au kwa wazazi na walezi, hivyo jukumu hilo haliwezi kukwepeka,” anasema Jokate na kutoa rai kwa wazazi na walezi kuufanyia kazi ushauri huo.

Ikumbukwe kuwa ushauri wake unakuja wakati sahihi ambao kama taifa, Tanzania ipo katika kazi kubwa ya kujenga jamii yenye maadili bora kutokana na uwepo wa mmomonyoko wa maadili. Iwe ni kiu ya kila mzazi na mlezi na mwana jamii kuona watoto wake wanakuwa na tabia njema. Kama msingi na kiwanda cha malezi ambacho ni familia kikiyumba na kushindwa kutimiza majukumu yake ya kimalezi ipasavyo, mmomonyoko wa maadili utaendelea.

Hata hivyo, wazazi na walezi wakirudi katika nafasi zao za kusimamia malezi ya watoto kuna ushindi kwani bado wanayo nafasi ya kuokoa kizazi hiki na kijacho, wakumbuke kuwa hawajachelewa.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0620 800 462.***

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Wadau wanapoandaa 'pepo' ya wabunifu, ila wasichana...

KATIKA dunia ya leo, ubunifu na utafiti ni muhimu kwa kuwa ndizo njia kuu za kutatua changamoto kuanzia za kiuchumi, ajira, afya na lishe bora vyote vikifungua milango ya maendeleo na maisha bora.

Leo, Tanzania haijabaki nyuma vijana kutoka maeneo mbalimbali wamekuwa wakiibua mawazo ya ubunifu yanayohitaji kukuzwa ili yalete tija kwao, jamii na taifa kwa kufanikisha kuwapo uzalishaji, ajira, bidhaa na huduma kwa kuamini kuwa bila kuendeleza kazi za ugunduzi na ubunifu pengine kusingekuwa na magari, ndege, simu za mkononi na meli.

Sifa mojawapo za wabunifu ni pamoja na kuwa wadadisi, wasioogopa kukosea na kukosolewa kwa kuwa bila kufanya majaribio na kushindwa huwezi kujifunza na hatimaye kufaulu.

Vilevile wabunifu hawaogopi kukosea kwa sababu wanajua kushindwa ni kati ya madaraja ya mafanikio, hawakubali hali ya kitu kama kilivyo bali wanatafuta njia za kukiboresha zaidi na zaidi.

Katika karne hii ya sayansi na teknolojia, mwamko wa vijana kuwa wabunifu unazidi kuongezeka na kuwafanya wadau kujitosa kuboresha ubunifu wao ili uweze kuwanufaisha.

Miongoni mwa wadau hao ni Kampuni ya Sahara Ventures ya Dar es Salaam, inayojishughulisha na ubunifu, teknolojia, ujasiriamali na uwekezaji, ambayo imejitosa kuboresha mawazo na ubunifu wa vijana nchini.

Ofisa Uendeshaji Mkuu wa Sahara, Musa Kamata, katika maelezo yake wakati wa maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, anaelezea jinsi wanavyojishughulisha na ukuzaji wa mawazo ya ubunifu ya vijana.

Kamata anasema jukumu lao ni kutoa mafunzo ya ubunifu na kuendeleza mawazo ambayo vijana wanayafikisha kwao kwa lengo la kuyakuza ili yawe na tija katika ubunifu.

"Yaani sisi tunachakata wazo hadi linakuwa na matokeo chanya. Ni sawa na mtu anayekuja hajui kusoma na kuandika tunamfundisha hadi anajua, ndivyo tunavyofanya katika kukuza ubunifu wa vijana," anasema.

Anafafanua wanafanya shughuli zao kwa kushirikisha Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), na kwamba kazi zinatambulika na wamekuwa wakitumiwa kutoa utaalamu katika mashindano ya kitaifa ya wabunifu.



Musa Kamata akiwaelezea viongozi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa jinsi Sahara Vantures inavyojishughulisha na ubunifu. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Kwa ujumla ni kwamba tunafanya kazi kwa karibu na COSTECH kuhakikisha tunainua ubunifu wa vijana wetu waweze kuwa na mchango katika maendeleo ya taifa lao," anasema.

Anasema kampuni hiyo ina vijana zaidi ya 5,000 ambao baadhi wamefika katika ofisi za Sahara jijini Dar es Salaam kupata mbinu za kukuza ubunifu wao na wengine wamefuatwa huko waliko.

"Sahara tuna vijana wengi nchi nzima wakiwamo walioko vyuoni. Kwa mfano tuna wasomi 30 katika vyuo vikuu vya Iringa, Sokoine Morogoro na Mandela Arusha ambao tunawafuata huko kuwapa mafunzo," anasema Kamata.

Anafafanua kuwa katika vyuo hivyo kuna vijana 10 kila chuo na pia wana vijana 100 katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Katavi ambao nao Sahara imewapa mafunzo ya kuendeleza ubunifu wao.

Ofisa huyo anataja vyuo vingine ambavyo kampuni yake inashirikiana navyo kuibua na kuendelea kuuhisha mawazo ya vijana kuwa halisia ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na cha Zanzibar (SUZA).

**NDOO MBOVU NI MALI**

Anatolea mfano moja ya ubunifu wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iringa, kwamba walikuja na wazo la kutengeneza namba, herufi na vibao vya kuandikia wanafunzi shuleni kwa kutumia ndoo mbovu za plastiki.

"Wazo lao lilikuwa ni kunitumia ubunifu huo kukabiliana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji wa ndoo za plastiki ovyo na pia kupunguza uhaba wa nyenzo za kufundishia katika shule za msingi," anasema.

Kiongozi wa wanafunzi walioshiriki ubunifu huo Bales Francis, anasema umechangia kupunguza tatizo la uchafuzi wa mazingira katika mji wa Iringa na pia kupunguza tatizo la nyenzo za kujifunzia.

"Kwa sasa tunahudumia shule 16 ambazo tunaziuzia vibao vya herufi, namba na vya vya kuandikia, kwani sisi ambao tumesoma shule za kayumba tunajua changamoto zake," anasema Francis.

Anafafanua kuwa vibao vya herufi kuanzia A hadi Z, zinauzwa kwa Sh. 10,000, wakati namba kuanzia 0 hadi 9 zinauzwa kwa Sh. 8,000 na kibao chenye ukubwa wa sentimita 35x20 kwa ajili ya kuandika, wanakiuza kwa Sh. 5,000.

"Katika ubunifu huu tuna mwaka mmoja na tumeanza kupata wateja kutoka nje ya mkoa wa Iringa na sasa wapo wa mikoa ya Njombe, Rukwa, Dar es Salaam na Mara," anasema.

> Tulikuja na ubunifu huu Sahara Vantures wakatuelekeza jinsi ya kufikia lengo na sasa tunaendelea na kazi ya kubuni vitu vingine zaidi huku tukitoa elimu, katika shule za sekondari Dar es Salaam.

**KUPITIA KATUNI**

Mmoja wa wanachama kutoka Shirika la Tai Tanzania ambalo ni matunda ya Sahara Vantures, Noria Madawili, anasema wao wamebuni katuni iitwayo Chapa Tatu ambayo wanaitumia kutoa elimu shuleni.

"Shirika letu la ubunifu, linajishughulisha kutoka elimu kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni, ukeketaji, hedhi salama, umuhimu wa elimu na masuala ya mabadiliko ya tabianchi," anasema Noria.

Anafafanua kuwa wamekuja na ubunifu huo baada ya kwenda katika maeneo ambayo yameshamiri vitendo vya ukatili wa kijinsia na kujionea hali ilivyo, kisha wakaitengenezea katuni ili kuelimisha wanafunzi.

"Huwa tunakwenda katika shule za sekondari za jijini Dar es Salaam na kuomba kukutana na wanafunzi sehemu ya wazi na kutoa elimu kupitia katuni hiyo," anasema.

Anasema katuni hizo zinaonyesha madhara ya vitendo hivyo na umuhimu wa elimu na kwamba kwa njia hiyo wanafunzi wamekuwa na uelewa mkubwa na kutambua mbinu za kuwa makini katika suala la mimba na ndoa za utotoni na pia kutambua umuhimu wa elimu na hedhi salama.

"Tulikuja na ubunifu huu Sahara Vantures wakatuelekeza jinsi ya kufikia lengo na sasa tunaendelea na kazi ya kubuni vitu vingine zaidi huku tukitoa elimu, katika shule za sekondari Dar es Salaam," anasema.

**WASICHANA NYUMA**

Pamoja na kupata idadi kubwa ya vijana wanaojifunza mambo ya ubunifu, Kamata anasema asilimia kubwa ni wa kiume, na kwamba wa kike bado wako nyuma na sababu kubwa ni mila na desturi.

"Katika maisha ya kila siku, wasichana wamekuwa nyuma katika ubunifu, kati ya vijana zaidi ya 5000 wanaojishughulisha na ubunifu chini ya kampuni ya Sahara Vantures, wasichana ni asilimia 25 tu ambao idadi yao ni ndogo huku wa kiume wakiwa wengi," anasema.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Ni miaka 50 ya mapinduzi ya simu duniani zikianzia Amerika

• 'Mshindi' hadi Nokia 3310 leo zipo kila aina, hata feki

MIAKA 50 tangu simu ya kwanza ya mkononi igunduliwe kifaa hicho kimebadilika na kuboreshwa na kuwa mahiri zaidi.

Kwa mujibu wa makala ya BBC ya Aprili mwaka huu, simu ya kwanza ya mkononi ilipigwa na Martin Cooper Aprili 1973, huko jijini New York, Marekani. Akipewa jina la utani la 'baba wa simu ya mkononi', Martin alivumbua Motorola DynaTac 8000 X, aliyoishikilia ikipewa jina la 'the Brick' Ni kwa sababu ya ukubwa.

Na hapa Tanzania itakumbukwa kuwa simu kubwa ziliitwa mshindi zikilinganishwa na mche wa sabuni ya kufulia (siyo sehemu ya makala ya BBC).



Martin Cooper aliyetengeneza simu ya kwanza ya mkononi akionyesha kazi zake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Simu hiyo kwa mujibu wa makala hiyo, ilizinduliwa 1983 na ilikuwa ya kwanza ya mkononi ambayo watumiaji wa kawaida waliinunua kwa gharama ya takribani Pauni £2,500. Ambayo kwa fedha za Tanzania kwa thamani ya sasa ingeweza kufikia Shilingi milioni 7.5.

Simu hiyo kwa kuwa kubwa na uzito kama begi dogo ilimaanisha kuwa haiwezi kuwekwa mfukoni hasa wa suruali kama vile simu za siku hizi zinavyobebwa kwenye mifuko ya shati na suruali kwa wanaume.

Ugunduzi uliendelea kufanikisha ujio wa simu nyingine kubwa ikiitwa IBM Simon inayochukuliwa kuwa mahiri na ya kwanza duniani, ingawa neno simu mahiri halikutumika wakati huo BBC inasema, ilitolewa mnamo 1993 na ilikuwa na kioo au 'skrini' nyeusi na nyeupe ya kupapasa au (touch xcreen).

Ugunduzi uliendelea na kabla ya miaka ya 2000 kampuni ya Nokia ya Finland ilitoa simu maarufu ya 3310. Iliyojulikana kwa muundo wake wa kudumu na pia ikielezwa kuwa ilikuwa na maisha marefu na betri yake ikiishi na chaja kwa siku kadhaa.

Aidha, ikafuatiwa na Nokia 1100 inasomwa (eleven hundred), mwaka 2003.

Mabadiliko kwenye sekta ya simu yakafuatiwa na ujio wa zile za kukunja na kukunjua 'clam shells' wengine wakiita 'flip flop' iliyokuwa maarufu sana mwanzoni mwa miaka ya 2000, mojawapo ni ' Motorola Razr V3.'

Teknolojia na ubunifu uliibua 'Blackberry' zilizojulikana zaidi kwa 'key board' zinazofanana na za kompyuta au kompyuta ndogo (mpakato). Zilikuwa maarufu sana kwa biashara kwani zilikuwa mojawapo ya simu za kwanza ambazo ungeweza kutuma barua pepe na kuandika kazi harakaharaka kama vile ambavyo ungefanya kwenye kompyuta mpakato.




Simu pendwa Nokia iliyobamba mioyo ya wengi.

Kuwapo kwa vipengele kama vile huduma ya kutuma ujumbe mfupi SMS, ilimaanisha kuwa umma kwa ujumla ulizipenda simu hizo

Ujio wa IPhone au 'apple' ulibadilisha kabisa dunia au ulimwengu wa simu za mkononi ikitolewa mwaka wa 2007 na Apple, teknolojia yake yenye 'skrini' ya kupapasa simu janja hiyo ilifanikisha kufikia mafanikio makubwa kwenye anga za mawasiliano ya kidijitali.

Siku hizi, simu za mkononi zinaendelea kuboreshwa na kurudi hata kwa mtindo na mwonekano wa zamani lakini kama kawaida kinachotikisa kinaweza kuwa ni mapenzi ya watumiaji kwa vile wanatamani kuwa na simu inayotumiwa kwa wepesi bila usumbufu mwingi.

Simu hizo rafiki wa mtumiaji au 'user friendly' zipo Samsung kuanzia Galaxy lakini ukweli ni kwamba unaweza kukosa pesa mfukoni lakini dunia ya leo inakuwa vigumu kukosa simu mkononi, hata kama wapo ambao hawana ni wachache na kwa nadra.

Kwa ujumla nchi ya kwanza kutumia simu ya mkononi ni Marekani iliyoanzishwa na John Mitchell na Martin Cooper wa kampuni ya Motorola mnamo 1973, siku hiyo ikielezwa kuwa ilikuwa na uzito wa kilo mbili, imeendelea kufanyiwa ubunifu na kuboreshwa zaidi.

Simu pendwa zaidi duniani kwa uzuri, rangi ya kioo au skrini ni jamii ya Samsung Galaxy, ikitengenezwa na kampuni ya Korea Kusini inasifika kuwa mojawapo wa wazalishaji wakubwa wa vifaa vya kielektroniki duniani. Lakini ipo Huawei Mate 4 inayotengenezwa China.

Afrika licha ya kuwa nyuma kielektroniki inaelezwa ndani ya ripoti ya Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AD) kuwa ina watumiaji wa simu milioni 650 barani Afrika ambao wanapita idadi hiyo nchini Marekani au Ulaya.

Inaendelea kusema kuwa katika baadhi ya nchi za Afrika watu wengi zaidi wanaweza kuwa na huduma za simu za mkononi iwe mijini au vijijini ikilinganishwa kupata maji safi, akaunti ya benki au umeme, mashirika hayo yanaongeza.

## Rais Samia alivyowaokoa mamia wasiliwe na wanyama hatari

**INATOKA UK.11**

Anazitaja shule mpya mbili za msingi ambazo zimejengwa, kuwa ni Nguzombili iliyopo Kata ya Maganzo na Winenekeja katika kata ya Igaga, na kwamba lengo la ujenzi wa shule hizo mbili katika maeneo hayo ni kusogeza huduma ya elimu karibu na wananchi.

Mkude anaeleza kuwa katika fedha hizo bilioni 40.4 zilizotumika kutekeleza miradi ya sekta ya elimu msingi katika mwaka wa fedha 2021/2022 wakati 2022/2023 Sh. bilioni 3.1 zilitumiwa.

Mkude anasema pia katika kuondoa tatizo hilo la wanafunzi kusoma umbali mrefu hasa wa madarasa ya chini, wamejenga shule shikizi (chekechea) tano, katika vijiji vya Ndema, Bubiki, Mizanza, Wizunza na Ijimija.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme, anawaambia wananchi kuwa serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imetoa Shilingi bilioni 52 kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu, ikiwamo na ujenzi wa shule mpya ambazo zitaondoa changamoto ya wanafunzi kusoma umbali mrefu.

Aidha, anawapongeza pia wananchi kwa kuguswa na suala la elimu na hata wengine kuanzisha ujenzi wa shule mpya ikiwamo Sekondari Nyahanga wilayani Kahama, kwa kuanza na ujenzi wa vyumba sita vya madarasa na serikali kujenga vingine nane na kufikisha vyumba 14 ambayo mwakani vitaanza kutumika.

Anaahidi kuwa serikali itaendelea kutatua changamoto katika maeneo yote ambayo wanafunzi wanasoma umbali mrefu ili wasome karibu na makazi yao na kufanya vyema kitaaluma kwa sababu wanakuwa na muda mwingi wa kujisomea.



## HABARI DODOMA

# VETA sasa yageukia mafunzo umeme jua

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imeanza kutoa elimu ya nishati ya umeme jua katika vyuo vyake vyote nchini.

Hatua hiyo ni moja ya njia za kuunga mkono jitihada za serikali za kuhakikisha nchi inapata umeme wa uhakika.

Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Kati, John Mwanja, akizungumza juzi wakati akifunga mafunzo ya nishati ya umeme jua ya wiki mbili kwa walimu wa vyuo 12 vya VETA ambayo yameandaliwa na VETA Singida kwa kushirikiana na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), alisema mafunzo hayo ni ya muhimu hasa katika kipindi hiki ambacho nchi ina mgawo wa umeme.

Mwanja alisema kupitia wahitimu hao, sasa VETA itapata walimu wa kufundisha kozi hiyo na kwamba mafunzo hayo awamu ya kwanza na ya pili yamefanyika hapo na kwa awamu hii waliona yasihusishe watu wa kutoka Singida pekee.

Alisema jukumu la VETA ni kufundisha ujuzi na elimu hiyo ya nishati ya umeme jua ni mwelekeo na mpango wa serikali kutokana na kuwepo kwa changamoto kubwa ya umeme na moja ya maono ya serikali ni kuona nchi inapata umeme kutokana na mfumo wa jua.

"Haiwezekani wataalamu hao wapatikane kwa kutumia kituo cha Singida peke yake, hivyo VETA wajibu wetu ni lazima wataalamu hao wasambae nchi nzima," alisema.

Mwanja alisema mahitaji ya VETA ni kutaka kila kijana aliyeko Busokelo mkoani Mbeya, kwa mfano, apate elimu hiyo katika vyuo vilivyoko katika eneo husika badala ya kwenda Singida jambo litakalowapunguzia gharama.

Alisema kutokana na hali hiyo, VETA iliona licha ya kozi hiyo kuanza kutolewa mkoani Singida, sasa itolewe katika mikoa yote kupitia vyuo vya VETA ili kuwasogezea huduma Watanzania.

Mwanja aliwataka wahitimu hao mara watakaporudi kwenye vituo vyao wakawe na mwendelezo wa kwenda kutoa elimu hiyo ambayo pia wanafunzi wanaojifunza fani ya umeme wa kawaida katika chuo hicho wameyapata.

Pia alivitaka vyuo hivyo kujitangaza ili shughuli wanazozifanya zifahamike ikiwa ni pamoja na mafunzo ya nishati ya umeme jua jambo litakalosaidia kufahamika na akahimiza pia kuanzisha kozi fupi za mafunzo hayo.

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo cha VETA Mkoa wa Singida, Alphonsina James, aliwashukuru washiriki wa mafunzo hayo kwa ushirikiano mkubwa walioonesha wakati wa mafunzo na kueleza kuwa kwao ni bahati kubwa kwani katika vyuo 48 ni vyuo 15 pekee ndio vilivyotoa washiriki hao.

Katika risala ya wahitimu hao kwa mgeni rasmi waliomba muda wa mafunzo uongezwe pamoja na uratibu wake ufanywe na VETA makao makuu kwa ajili ya uwezeshwaji ambapo pia waliomba kuwezeshwa vifaa vya kufundishia.

# Wataka wazee wabakaji wasionewe haya

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

CHAMA cha Wazee Wanaume Tanzania kimeiomba serikali kuwachukulia hatua wazee wanaobainika kuwabaka watoto na wajukuu kwa imani ya ushirikina.

Mwenyekiti wa chama hicho, Joseph Laizer, alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa chama hicho uliofanywa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.

"Tunaomba serikali kutowaonea huruma na aibu kwa wanaojihusisha na vitendo vya ubakaji wa watoto na tunataka wachukuliwe hatua kali ikiwamo vifungo vya maisha. haiwezekani wazee ambao ndio tegemeo kubwa katika kuelimisha vijana na watoto katika malezi bora, wafanye vitendo vya ovyo," alisema.

Akizindua chama hicho, Dk. Gwajima alivitaka vyama vinavyoshughulika na masuala ya wazee nchini kufanya kazi kwa karibu na mabaraza ya kisera ya wazee kupitia mwongozo wa kitaifa uliozinduliwa Oktoba 6, mwaka huu, kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Geita.

Pia alisisitiza asasi na vyama hivyo kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sera, sheria, miongozo na mipango ya serikali huku zikizingatia katiba zao bila kuingilia majukumu ya mamlaka zingine au vyama vingine na kuwa na mikakati ya kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao kikamilifu.

Kuhusu kudhibiti mmomonyoko wa maadili, Waziri Gwajima alisema chama hicho pia kina wajibu wa kuchochea malezi chanya ya watoto na vijana, huku wajumbe wa chama hicho wakiwa mfano kuwajibika kukemea mmomonyoko wa maadili katika jamii unaosababishwa na kukosa malezi stahiki.

Aidha, kwa kushirikiana na majukwaa ya wazee, serikali imefanya mapitio ya Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 na kuja na rasimu ya sera ambayo iko hatua za mwisho.



Wajumbe wa mkutano wa Chama cha Wafugaji kutoka mikoa mbalimbali wakimsikiliza Mwenyekiti wao, Mrida Morocha (hayupo pichani), kuhusu uzinduzi wa kadi mpya ya elektroniki uliofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wafugaji wasisitizwa kufuga kwa tija

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

SERIKALI imewataka wafugaji kufuga kwa tija badala ya kuendelea kuwa na makundi makubwa ya mifugo ambayo ni mzigo pindi yanapokosekana malisho.

Kaimu Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alitoa maagizo hayo jana alipokuwa akizungumza na wafugaji kutoka Tanzania Bara kwenye mkutano mkuu wa uzinduzi wa kadi za kielektroniki za wanachama wa Chama cha Wafugaji Taifa (CCWT), uliofanyika jijini hapa.

Alisema ufugaji huo waliouzoea wa kuwa na makundi mengi umekuwa ukiwasababishia kukosa maeneo ya malisho na kwamba hali hiyo inawafanya kujikuta kwenye migogoro kati yao na upande wa serikali na wakulima inayotokana kuchunga kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

"Migogoro mingine inaweza kuepukana pale wafugaji wenyewe watakapopunguza mifugo hiyo na hata maeneo ya kuchunga yatakuwa yanajitosheleza kutokana na mifugo hiyo kutokuwa mingi kama ilivyo sasa kwa kuwa baadhi ya wafugaji wana mifugo mingi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa CCWT, Mrida Marocho, alisema bado wafugaji wanakabiliwa na kero ya kukamatwa mifugo yao na viongozi wa serikali kwa kuonewa hali ambayo inayoendelea kusababisha migororo.

Alisema wafugaji wamekuwa wakikamatwa kwa kushinikizwa na baadhi ya viongozi hao wa serikali ili wapatiwe mamilioni ya fedha, hali ambayo imekuwa ikichochea kuwapo kwa migogoro mikubwa kwenye maeneo wanayoishi.

Mwenyekiti huyo alisema kutokana na kuwapo kwa mgogoro kati ya wafugaji na viongozi hao wa serikali, chama kinaomba kuona namna bora ya kuwakutanisha na wakuu hao ili kutatua migogoro pale mifugo inapoingia kwenye maeneo yasiyoruhusiwa yakiwamo ya hifadhi.

"Kwa kuthibitisha hilo, hivi karibuni kuna zaidi ya ng'ombe wapatao 100 wanashikiliwa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Tunduru mkoani wa Ruvuma hali ambayo inasababisha usumbufu mkubwa kwa madai kuwa mifugo hiyo iliingia katika maeneo ya hifadhi," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, chama kinaomba serikali kuona namna bora ya mifugo hiyo kuachiwa badala ya kuendelea kushikiliwa huku wakitaka mamilioni ya fedha kutoka kwa mfugaji huyo.

Kuhusu uzinduzi wa kadi hizo, mwenyekiti huyo alisema wafugaji watanufaika kupitia usajili huo na pia watatambuliwa kwa idadi yao pamoja na mifugo kama inavyohitaji serikali kuwaboreshea sekta nzima ya ufugaji.

Aliwahimiza wafugaji kujiandikisha kwenye chama ili kupata usajili wa kadi hizo ambazo zitaenda kuwasaidia kupata mikopo kwenye benki ya CRDB waliyoingia nayo mkataba.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho, Busundwa Wamarwa, aliwataka wafugaji wawekeze kwenye viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya mifugo yao.

Pia alisema maeneo mengi ya ufugaji yanakabiliwa na tatizo kubwa ya uhaba wa maji hivyo wakipata kadi hizo na kusajili wanaweza kupatiwa mikopo ambayo itawainua zaidi kiuchumi kupitia mifugo yao.





# RUWASA yaagizwa kuvunja mkataba mradi Madibila

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

WIZARA ya Maji imemwagiza Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Hance Patrick, kuvunja mkataba wa mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wa Madibila kutokana na kusuasua.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika eneo hilo kukagua maendeleo ya mradi ambao unaotekelezwa kwa zaidi ya Sh. milioni 800.

Mahundi alisema mkandarasi huyo mzawa anaharibu nia ya serikali ya kuanza kuwapa kipaumbele makandarasi wazawa kwa maelezo kuwa mpaka sasa mradi huo ulitakiwa uwe umekamilika, lakini hajafikisha hata asilimia 30.

Alisema wizara yake inafuatilia miradi yote, lakini mradi huo umekuwa ukisuasua kutokana na uwezo mdogo wa mkandarasi huyo na kuwasababishia wananchi kuchelewa kupata huduma hiyo muhimu.

"Tumekuwa tukitaka kuwatumia makandarasi wazawa ili fedha zetu zizunguke humuhumu, lakini mkandarasi huyu ametukera mpaka sisi wizarani, nakuachia hili Injinia Hance meneja wa RUWASA mkoa, hili liko ndani ya uwezo wako," aliagiza Mahundi.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Samwel Hachei, alisema mkandarasi anayetekeleza mradi huo ni Kampuni ya Amtec Consulting yenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam na mkataba wake ulikuwa wa mwaka mmoja pekee.

Alisema mkataba wa mkandarasi huyo ulikuwa unaisha Oktoba 27, mwaka huu, lakini mpaka sasa umekamilika kwa asilimia 25 huku mkandarasi huyo akiomba kuongezewa muda wa utekelezaji.

Alisema mradi huo ukikamilika utakuwa unawanufaisha zaidi ya wananchi 18,000 wa vijiji vitano vya kata hiyo ya Madibila ambao kwa sasa wanahangaika kupata huduma hiyo kwenye maeneo ambayo hawana uhakika wa usalama.

"Mpaka sasa mkandarasi huyu tumeshamwandikia barua ya kukusudia kuvunja mkataba ili tutafute njia mbadala ya kukamilisha mradi huu na wananchi waanze kupata huduma," alisema Mhandisi Hachei.

Mbunge Mteule wa Jimbo la Mbarali, Bahati Ndingo, aliiomba serikali kutumia njia mbadala kukamilisha mradi huo ili wananchi waondokane na adha ya kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo kwenye maeneo ambayo siyo salama.

Alisema fedha ambazo serikali imezitoa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo ni nyingi na kutakiwa usimamizi wake uwe madhubuti ili matokeo chanya yapatikane.

Diwani wa Kata ya Madibila, Selemani Msiminyungu, alisema mbali na mkandarasi huyo kuchelewa kukamilisha mradi huo pia ana tatizo la kutowalipa wafanyakazi wake hali inayoweza ikasababisha wizi wa vifaa vya ujenzi.

Aliiomba serikali ivunje mkataba huo haraka na ikiwezekana watekeleze RUWASA kupitia mfumo wa akaunti ya dharura (Force account) ili ukamilike haraka.

Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa zenye tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama hasa ya bomba jambo ambalo linawalazimu wananchi kutumia kutoka kwenye vyanzo ambavyo siyo vya uhakika.



Wachuuzi wa matikiti maji katika Soko la Simu 2000, Sinza, Dar es Salaam wameuomba uongozi wa Manispaa ya Ubungo kuwaleta wafanyabiashara kutoka masoko mengine ili soko lao liweze kuchangamka. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mkandarasi apewa mwezi kukamilisha nyumba za watumishi

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

KAMATI ya Fedha, Uongozi na Mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, imetoa mwezi mmoja kwa mkandarasi anayejenga nyumba ya kuishi watumishi wa Kituo cha Afya cha Itale wilayani humo ili ianze kutumika.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Tata Kibona ambaye ni Diwani wa Kata ya Ibaba, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema jengo hilo ambalo litakuwa linatumiwa na familia mbili linatakiwa limamilike kabla ya Desemba na endapo halitakamilika watachukua hatua kali dhidi ya mkandarasi aliyepewa tenda hiyo.

Kibona alisema ripoti ya mwenendo wa ujenzi wa jengo hilo imebainisha kuwa kasi ya mradi huo ni ndogo na haiendani na mahitaji halisi ya mradi huo.

"Mradi huu ni wa muda mrefu na pesa tayari ilishatengwa kwa ajili ya kuhakikisha jengo hili linajengwa kwa kasi na linakamilika kwa wakati ili watumishi wetu waanze kuishi hapa badala ya kuhangaika kwenye nyumba za kupanga," alisema Kibona.

Alisema kwenye ukaguzi wao walibaini kuwa kazi inafanyika, lakini kwa kusuasua kiasi kwamba mradi unaweza kuchelewa kukamilika na watumishi hao wakawa wanaendelea kuhangaika.

Ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali inaendelea katika maeneo tofauti ya Wilaya ya Ileje, lengo ni kuhakikisha kamati inasaidia katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya serikali ambayo inatumia pesa nyingi ili kuwaletea maendeleo wananchi wake.

**Kibona alisema ripoti ya mwenendo wa ujenzi wa jengo hilo imebainisha kuwa kasi ya mradi huo ni ndogo na haiendani na mahitaji halisi ya mradi huo.**

# Usafirishaji haramu binadamu washamiri nchini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la usafirishaji haramu wa binadamu linaendelea kushamiri nchini baada ya watu 11 raia wa Ethiopia kukamatwa na polisi mkoani Mbeya wakisafirishwa kuelekea nchini Malawi huku wakiwa hawana vibali vya kuingia nchini.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema watu hao walikamatwa Oktoba 27, mwaka huu katika eneo la Igawa wilayani Mbarali katika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Kamanda Kuzaga aliwataja watu hao kuwa ni Mulatoto Amdado, Nugushi Handibal, Aulosy Segea, Takatary Mwanjiso, Goodso Bekere, Lamborn Ondose, Ndale Kermah, Kibiruh Tamrah, Tafasah Alarm, Mestin Tasfay na Chalu Ababa.

Alisema watuhumiwa walikuwa wakisafirishwa kwa kutumia gari ndogo yenye namba za usajili T.732 CRB aina ya Toyota Mark X rangi nyeupe ambayo ilikuwa ikiendeshwa na Frank Makunde (38), mkazi wa Makambako, Mkoa wa Njombe.

"Dereva huyu amekamatwa na hatua zaidi za kisheria zinaendelea kuchukuliwa, lakini pia tunaendelea na ufuatiliaji zaidi ili kuwabaini wasafirishaji wengine pamoja na mmiliki wa gari hii iliyokuwa inatumika kuwasafirisha watu hawa," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wananchi kuacha kujihusisha na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa kuwa ni kinyume cha sheria na kuonya wakikamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani na kufungwa gerezani.

Alisema kwa mujibu wa sheria, chombo chochote kinachotumika kusafirisha wahamiaji haramu, kinatakiwa kutaifishwa na kusisitiza kuwa gari iliyotumika kuwasafirisha watu hao itataifishwa na serikali.

Wahamiaji wengi wanaokamatwa mkoani Mbeya ni raia wa Ethiopia na Somalia na husafirishwa kwenda nchini Malawi na Afrika Kusini.

## Othman ataka utambuzi ardhi uharakishwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amewataka wasimamizi wa Sekta ya Ardhi kujitahidi kuharakisha na kukamilisha kazi za utambuzi wa ardhi ili kusaidia kudhibiti tatizo la migogoro ya ardhi inayoendelea kujitokeza.

Aliyasema hayo hayo alipotembelea eneo la Makaani Vitongoji, Mkoa wa Kusini Pemba baada ya malalamiko ya wananchi wanaotumia eneo hilo kwa shughuli zao za kijamii kudai kunyang'anywa ardhi katika eneo hilo waliyoitumia kwa muda mrefu bila kulipwa fidia.

Alisema kutokuwapo na utambuzi rasmi wa ardhi kisheria kunachangia migogoro mingi ya ardhi pamoja na manung'uniko makubwa ya wananchi kudhulumiwa jambo ambalo halipaswi kuendelea.

Alisema sekta ya ardhi ni eneo linaloendelea kuwa na changamoto kubwa wananchi kudhulumiwa na kudhulumiana jambo ambalo linawezekana kutatuliwa na kufanywa lisiendelea kujitokeza.

Kadhalika, alisema hivi sasa kunajitokeza eneo moja kutolewa hati nyingi za umiliki na kusababisha kuendelea kwa migogoro mikubwa ya ardhi jambo ambalo serikali haipendelei liendelee.

Aliwataka wananchi na viongozi mbalimbali waliohudhuria kikao hicho ni muhimu kwa wasimamizi hao kusimamia utaratibu kupitia sheria ya utambuzi wa ardhi ili kuondoa tatizo la wananchi wengi kuwa na haki ya matumizi ya ardhi bila kuwa na hati za umiliki.

Alisema hali hiyo inatoa fursa kwa wajanja kuendelea kuwadhulumu wananchi na kusababisha malalamiko dhidi ya serikali na watendaji wake jambo ambalo linaweza kudhibitiwa.

Aidha aliwataka viongozi katika sekta hiyo kuwapa wananchi ufafanuzi unaofaa pale wanapohitaji na ni vyema kutolewa kwa mujibu wa miongozo ya serikali na taratibu za sheria ya ardhi nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahor Masoud, alisema serikali ya Mkoa wake inajitahidi kufuatilia na kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi inayojitokeza katika mkoa wake ili kuhakikisha wananchi hawadhulumiwi haki zao.

Alisema kwamba mwongozo wa Rais Dk. Hussein Mwinyi ni kuhakikisha hakuna sehemu ya ardhi ya mwananchi inayochukuliwa kwa matumizi ya umma bila mmiliki halali kulipwa fidia.

Aliwataka wananchi kufuatilia kwenye mamlaka na vyombo vinavyosimamia ardhi kisheria lakini pia wanafika ofisi na wilaya na mikoa kutoa taarifa pale migogoro inapojitokeza na hatua kuchukuliwa.

Awali, wananchi wa eneo la Makaani Vitongoji walisema wamenyang'anywa ardhi walizozitumia kwa muda mrefu na kupewa baadhi ya kampuni na sehemu nyingine kukatwa viwanja na kupewa baadhi ya viongozi serikalini bila wao wenyewe kulipwa fidia.

# Miradi sekta ya uvuvi yaongezeka Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesema miradi ya sekta ya uvuvi imeongezeka kutoka mmoja hadi 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 337.5, kutoka Sh. bilioni 10 tangu Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuanzisha mpango wa uchumi wa buluu visiwani humo.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi na utekelezaji wa mpango wa uchumi wa buluu kupitia rasilimali za baharini.

Alisema miradi hiyo inajumuisha sekta ya uvuvi, mwani, ufugaji wa viumbe maji, viwanda vya kusarifu dagaa, ujenzi wa masoko na madiko (kambi), uhifadhi wa bahari, utafiti na kilimo na utafiti wa mafuta na gesi.

Alisema mpango wa uchumi wa buluu umelenga kukuza ubunifu na vipaumbele vikubwa vya kusaidia wajasiriamali zana za kujiongezea ajira, kuongeza thamani ya mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji na masoko pamoja na kusarifu mazao ya baharini chini ya mpango huo.

"Wakati serikali ya awamu ya nane inaingia madarakani uzalishaji wa samaki ulikuwa tani 38,107 zenye thamani ya Sh. bilioni 205.4 kwa mwaka, lakini sasa uzalishaji umefikia tani 61,794 zenye thamani ya Sh. bilioni 391.37 kwa mwaka," alisema Jumbe na kuongeza kuwa ongezeko hilo ni la kihistoria katika visiwa vya Zanzibar.

Alisema kimsingi sekta ya uvuvi Zanzibar, sasa inachangia Pato la Taifa (GDP) kwa mwaka asilimia 6.32 kutoka asilimia 4.5 kuanzia mwaka 2020 hadi 2022.

Alisema mafanikio hayo yametokana na jitihada na moyo wa kujitolea wa Rais Mwinyi baada ya kuamua kuleta mageuzi ya kiuchumi kupitia sekta ya uvuvi chini ya mpango wa uchumi wa buluu hatua ambayo imesaidia kuwainua wavuvi wadogo 50,000 katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema chini ya mpango huo kwa kushirikiana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sekta ya uvuvi wa bahari kuu imepata mafanikio makubwa baada ya leseni za uvuvi wa bahari kuu kufikia 100 zilizotolewa kwa meli za kigeni na za ndani hatua ambayo imesababisha mgao wa Tanzania kimataifa wa uvuvi wa samaki aina ya jodari kupindukiza tani 4000 kwa mwaka.

"Tumesharudi katika kamisheni ya kimataifa ya uvuvi wa jodari ya bahari ya hindi na kuomba kuongezewa mgao zaidi unaokwenda sambamba na kasi ya uchumi wa buluu," alisema na kuongeza kuwa tayari Tanzania imeingia ubia na kampuni za uvuvi wa kimataifa ikiwamo ya Albakora.

Aidha, alisema serikali katika kuwajengea uwezo wavuvi imewaondoa katika uvuvi wa mtu mmoja mmoja na kuwaingiza katika vya makundi kama wajasiriamali na kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba ili kushiriki katika uvuvi wa bahari kuu na kuwawezesha vifaa kama boti, mashine na vifaa vya usalama baharini.

Alisema wavuvi wamepatiwa boti 577 ambazo zitawanufaisha 50,000 wanaokwenda kuvua kila siku katika mwambao wa bahari ya Zanzibar na kupitia mradi wa kuimarisha sekta ya uvuvi Zanzibar inaofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), mipango ya ununuzi wa meli nne za uvuvi imewekwa na hatua ya ununuzi wa meli ya kwanza ya uvuvi yenye thamani ya Shilingi bilioni tano imeanza kufanyika.

"Kupitia kampuni ya ZANFRESH na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), meli ya uvuvi moja imenunuliwa na hatua zinazoendelea kufanyiwa ukaguzi kabla ya kuletwa Zanzibar kuanza kufanya kazi," alisema Jumbe.

Aidha, alisema tayari ZAFICO inamiliki meli mbili za uvuvi aina ya MV Sehewa namba mbili na namba tatu na tayari kampuni ya ZAFICO imeshaingia ubia na kampuni moja ya kimataifa kuendesha shughuli za uvuvi wa bahari kuu nchini.

Hata hivyo, alisema katika kuwapatia soko la uhakika wavuvi, soko la kisasa limejengwa likiwa na thamani dola milioni 14 katika eneo la Malindi, Unguja lenye uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi wapato 43,000 wakiwamo wavuvi, madalali, wauzaji, wachuuzi, washushaji na wabebaji wa samaki pamoja na kufunga mitambo ya baridi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 200 za samaki kwa wakati mmoja na mtambo wa kuzalisha barafu.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanikiwa kuimarisha sekta ya uvuvi Zanzibar baada ya kuivunja idara ya uvuvi na kuunda wizara maalum ya kusimamia sekta hiyo baada ya kuingia madarakani mwaka 2020.



Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kuhusu mafanikio ya wizara hiyo katika miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi afagilia mbio za Marathon

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mbio za Marathon zina faida ya kiafya, ajira na uchumi na hukuza sekta ya utalii.

Alisema hayo akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika msimu wa tatu wa mbio za Zanzibar International Marathon zilizoshirikisha wakimbiaji wa nchi mbalimbali za Afrika Mashariki, Ulaya na Amerika.

Alisema katika kuvutia wageni kipindi chote cha msimu mdogo wa watalii, lazima kuwa na utalii wa matukio ikiwamo Tamasha la ZIFF, Sauti za Busara, pamoja na matukio ya kimichezo ikiwamo mbio za Zanzibar International Marathon kwa kuhamasisha kufurika wageni vipindi vyote msimu mkubwa na mdogo wa utalii.

Aliwataka wananchi kufanya mazoezi kila wakati kwa kujiunga na vikundi vya mazoezi kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza yakiwamo shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo, saratani, kiharusi na mengineyo.

Aidha, alisema sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika nchi, asilimia 30 ya pato la taifa inatokana katika sekta hiyo.

Rais Mwinyi alisema Zanzibar inategemea utalii wa aina mbili; wa fukwe za bahari na wa masuala ya urithi unaotokana na majengo ya kihistoria.

"Nachukuwa fursa hii kuipongeza kwa dhati Zanzibar International Marathon kwa kuleta marathon hii na kubadilisha muda ambao walikuwa wanafanya miaka yote kuifanya katika miezi ambayo tulikuwa sisi tunaona tukiweka tutaondoa suala la msimu mdogo wa utalii," alisema.

Ofisa Mkuu wa Tigopesa kutoka Kampuni ya Tigo-Zantel, Angelica Pesha, alisema Tigo-Zantel wanajivunia kuwekeza Zanzibar ili kuhakikisha wateja wao wanafurahia faida ya teknolojia na kuboresha maisha yao ya kila siku.

Alisema mwaka 2022 walianza kuwekeza katika mradi wa kuimarisha miundombinu ya teknolojia ya mtandao wao, na wamekuwa kampuni ya kwanza ya mawasiliano Tanzania kuleta teknolojia ya mtandao wa 5G, yenye kasi zaidi visiwani Zanzibar.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Yussuf Juma Mwenda, alisema katika miaka mitatu ya uongozi wa Rais Mwinyi, imerahisisha shughuli za kiuchumi na matamasha mbalimbali huchangia katika uimarishaji huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



JERRY WILSON anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0358-0142 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SHIGHATINI SEKONDARI mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: WMB/RB/2851/2023.

## KUPOTEA KWA CHETI



**MEDIKUS WILBARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S963-0232** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KISHANDA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/32875/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**BEATRICE MANIMO ONA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5431/0010** kilichotolewa na **HARADALI WINNERS SEKONDARI** mwaka 2020. Result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.1442/0502** iliyotolewa na MWANDET HIGH SCHOOL mwaka 2023. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **PHQ/DAR/UBU/32242/2023 na PHQ/DAR/UBU/32239/2023.**

FOMU MIRATHI - 3

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya RUFIJI**

**Kituo cha IKWIRIRI Mkoa wa PWANI**

**Shauri la madai/Ndoa Na. 32/2023**

**Jina la Mdai SARAH GODSON MSHEWA**

**Jina la Mdawia DAVID CHACHA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: DAVID CHACHA**
**MARA MUSOMA**

**Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**MADAI YA KUVUNJA NDOA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 15 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa.....asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Mwezi 10 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **GS GROUP LTD.** aina ya **HAOJUE** namba za usajili **MC761DSH.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/6001/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **GS GROUP LTD.** aina ya **HAOJUE** namba za usajili **MC761DSH.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/6001/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **GS GROUP LTD.** aina ya **HAOJUE** namba za usajili **MC993DSJ.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/6001/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **GS GROUP LTD.** aina ya **HAOJUE** namba za usajili **MC721DSH.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/6001/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



MOHAMED S. NAMDIMBE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3488/0023 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ZIWANI SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/UBU/32800/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEREMANICO JOHN LIBORI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAUM** yenye usajili namba **T976CUV,** CHASSIS NAMBA: **NCZ200075719** na ENGINE NAMBA: **1NZB661303.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/32172/2023**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED**, I the undersigned **ELIZABETH JOSEPH MOLEL,** Christian, Female, an Adult and a Citizen of the United Republic of Tanzania of P.O. Box 229, Tanga, originally known as **ELIZABETH JOSEPH MULAL** as it is indicated in my National Identification Card and other documents, do hereby declare and absolutely renounce and abandon the use of my father name **ELIZABETH JOSEPH MULAL** and in lieu thereof do assume as from this date the name **ELIZABETH JOSEPH MOLEL** and in pursuance of such change of my name as aforesaid, I hereby declare that I shall, at all times hereinafter in all records, deeds, proceedings and instruments in writing and on all actions, and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **ELIZABETH JOSEPH MOLEL** as my name in lieu of my abandoned name of **ELIZABETH JOSEPH MULAL.**

**AND** I hereby authorize and request all persons to designate and address me by my assumed name of **ELIZABETH JOSEPH MOLEL.**

**IN WITNESS** hereof I have this 17th day of October, 2023 set my hand in the manner appearing hereunder:-

the manner appearing hereunder:-

SWORN at TUNDURU by the said ELIZABETH JOSEPH MOLEL who is known to me personally this 17th day of October 2023

DEPONENT



BEFORE ME:-
Name: Kolzlege Prosper
Signature:
Address: P.O Box 160, Tunduru
Occupation: COMMISSIONER FOR OATHS.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 132**

**KIKUNDI CHA SONGAMBELE**
**[SEVERIN ABEL MAHANO]............MDAI**

**VS**

**JUMANNE KIKOTI...............................MDAIWA**

**MAOMBI YA MADAI**

Unatakiwa katika Mahakama tarehe 9/11/2023 saa 2:30,asubuhi kwajili ya shauri lako la madai usipofika shauri lako litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uwamuzi

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 30/10/2023.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT MOROGORO**
**TAXATION CASE NO. 20 OF 2023**
**(Arising from Misc. Land Application Case No. 08 of 2023 From the High Court of Tanzania at Morogoro)**
**APEL PETROLEUM LIMITED...............APPLICANT**
**VERSUS**
**STARCOM CONSUMER HEALTHCARE LIMITED......1ST RESPONDENT**
**HENRY ABSALOM VEGULA..................2ND RESPONDENT**
**NOTICE TO APPEAR**
**SUBSTITUTED SERVICE**
**[Made under Order V rule 16 of the Civil procedure Code, Cap. 33 R.E 2019]**

**TO:**
**STARCOM CONSUMER HEALTHCARE LIMITED.**

**TAKE NOTICE** that the above named Applicants has instituted Taxation Cause against you and the same is fixed for Hearing on 02nd day November, 2023 at 09:30 A.M, before **Hon. A. W. MMBANDO, DR.** in the High Court of Tanzania at Morogoro.

You are thus required to appear in person or through your Advocate or dully authorized agent without fail.

**TAKE FUTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on the afore mentioned date and time, the Court shall proceed to hear and determine the case in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of this **COURT** this 16th October, 2023.

..............................
**DEPUTY REGISTRAR**
**MOROGORO**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE No 109 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE:**
**WINFRIDA KISEKE HONGOA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**

**1: LAZARO WILLIAM MPAKI**
**2: ......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 02 day of 11.2023

DATED at MOROGORO this 23 day of 10.2023

..................................................
**Resident Magistrate**

**Jamhuri Ya Muungano Wa Tanzania**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KILINDI**
**RUFAA NA.47 YA MWAKA 2019**
**HATIBU SEMDILI MAGUWO...............MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**RAJABU SAIDI ..................................MJIBU RUFAA**

**KWA, SAIDI RAJABU POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

HATIBU SEMDILI MAGUWO alikata Rufaa dhidi ya baba yako ambaye kwa sasa ni Marehemu mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) kilindi Tanga lililopo Songe. Rufaa hii imepangwa kusikilizwa 13/11/2023 saa tatu asubuhi mbele ya Mh Mhina ER, Mwenyekiti.

Hivyo basi ukiwa kama motto wa marehemu RAJABU SAIDI unatakiwa kufika wewe au wakili wako kwa tarehe iliyopangwa kuendelea na shauri aliloacha baba yako. Vielelezo kuhusu shauri hili vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Kilindi. Endapo hautatekeleza haya shauri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa baraza la ardhi na Nyumba Wilaya ya kilindi leo 16/10/2023.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KILINDI**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**CIVIL REFERENCE NO. 3 OF 2023**
*(Arising from Civil case No. 21 of 2022 in the District Court of Arusha at Arusha, originating from Arusha Urban Primary Court in Civil case No. 103 of 2021)*

**AMANI YONA MOSES ................................................ APPLICANT**
**VERSUS**
**LONG'IDA LEWAWO ............................................1ST RESPONDENT**
**NANG'UTUTI SIMANGO..........................................2ND RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

TO;

2. NANG'UTUTI SIMANGO

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing in the High court of Tanzania at Arusha on **10th** day of **November, 2023** at 09:30 a.m in the forenoon. You are required to appear in person.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for hearing, the court may proceed in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of the **COURT** this **17th** day of **October, 2023.**

**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT**
**ARUSHA**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**CIVIL REFERENCE NO. 3 OF 2023**
*(Arising from Civil case No. 21 of 2022 in the District Court of Arusha at Arusha, originating from Arusha Urban Primary Court in Civil case No. 103 of 2021)*

**AMANI YONA MOSES ................................................ APPLICANT**
**VERSUS**
**LONG'IDA LEWAWO ............................................1ST RESPONDENT**
**NANG'UTUTI SIMANGO..........................................2ND RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

TO;

1. LONG'IDA LEWAWO

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing in the High court of Tanzania at Arusha on **10th** day of **November, 2023** at 09:30 a.m in the forenoon. You are required to appear in person.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for hearing, the court may proceed in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of the **COURT** this **2rd** day of **October, 2023.**

**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT**
**ARUSHA**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Idadi waliokufa Gaza yafikia watu 8,000

**GAZA,** Palestina

KWA mujibu wa Wizara ya Afya ya Gaza iliyoko chini ya kundi la Hamas, zaidi ya watu 8,000 wengi wao wakiwa ni raia wa kawaida wameuawa tangu Israel ilipoanza kuushambulia kwa mabomu ukanda huo.

Wizara hiyo jana ilibainisha pia kuwa watu wanne wameuawa mjini Jenin katika eneo linalokaliwa kwa mabavu na Israel la Ukingo wa Magharibi wakati majeshi ya Israel yalipokabiliana na Wapalestina.

Aidha, wakati hayo yakielezwa, ilibainishwa kuwa wakazi wa Gaza wanaojihifadhi katika hospitali kubwa zilizo kwenye ukanda huo, wamejawa na wasiwasi baada ya Israel kutangaza uwezekano wa kufanya mashambulizi kwenye maeneo hayo.

Baada ya Jeshi la Israel kuwataka watu waliojihifadhi kwenye Hospitali ya Al Quds na katika Kitongoji cha Ta al-Hawa waondoke kwenye maeneo hayo, wakazi hao walielezea wasiwasi wao huku wakisema kuwa hawana pa kwenda.

**Shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu misaada ya kiutu na masuala ya dharura (OCHA) lilisema licha ya kiwango kidogo, bidhaa za misaada zilizopo zitakuwa na jukumu muhimu katika kuimarisha huduma ya afya mjini Gaza.**

Kwa mujibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Shirika la Msalaba Mwekundu ukanda wa Gaza, tayari Israel imefanya shambulio lililosababisha uharibifu katika maeneo jirani na hospitali hiyo.

Jeshi la Israel lilisema vikosi vyake vimeua makumi ya magaidi ambao walijificha katika majengo na mahandaki na kujaribu kuwashambulia wanajeshi wake ndani ya saa 24 zilizopita.

Ilielezwa kuwa katika moja ya mashambulizi hayo, ndege ya kijeshi ya Israel ililenga jengo lililokuwa na zaidi ya wapiganaji 20 wa Hamas ndani yake. Huku mfumo wa kuzuia makombora katika eneo la Chuo Kikuu cha Al-Ahzar katikati mwa mji wa Gaza kikitajwa kushambuliwa.

Pia ilibainishwa kuwa eneo hilo limekuwa kitovu cha mashambulizi ya Israel tangu shambulio la Hamas la Oktoba 7. Jeshi likisema kwamba lililenga zaidi ya maeneo 600 ya magaidi yakiwamo maghala ya silaha na maeneo iliko mifumo ya kuzuia makombora, maficho na maeneo yanayotumiwa na Hamas.

Wapiganaji wa kundi la Hamas wameripoti pia mapigano makali katika eneo hilo ikiwa ni usiku wa tatu tangu Israel ilipotanua operesheni yake ya kijeshi kwa kutumia vifaru na magari ya kivita ndani ya ardhi ya Gaza iliyoharibiwa vibaya kwa mashambulizi.

Hayo yakiendelea, Umoja wa Mataifa (UN) ulisema malori 117 yaliyobeba misaada yameingia Gaza tangu vita vilipoanza na kwamba misaada hiyo ni chini ya misaada yote inayohitajika.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu misaada ya kiutu na masuala ya dharura (OCHA) lilisema licha ya kiwango kidogo, bidhaa za misaada zilizopo zitakuwa na jukumu muhimu katika kuimarisha huduma ya afya mjini Gaza.

**WITO KWA ISRAEL**

Katika hatua nyingine, Rais wa Marekani Joe Biden, imeishinikiza Israel kuchukua tahadhari katika kuwalinda raia wa Gaza pamoja na kuongezwa mara moja msaada wa dharura, wakati kukiwa na kilio kutokana na idadi kubwa ya vifo na wanaojeruhiwa.

Wakati kiongozi huyo akizungumza na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, alisema licha ya haki ya Israel kulinda raia wake, lakini izingatie pia sheria za kimataifa kuhusu kulinda raia wengine.

Viongozi hao wawili walizungumza pia juu ya juhudi za kuwalinda takribani mateka 200 waliochukuliwa na kundi la Hamas tangu Oktoba 7, kutokana na shambulio lililosababisha vifo vya watu 1,400 ndani ya Israel.

Taarifa ya White House ilieleza kwamba Biden, alisisitiza juu ya umuhimu wa kuongeza kwa haraka na kwa kiwango kikubwa msaada wa dharura ili kukidhi mahitaji ya wakazi wa Gaza.

Ilielezwa kuwa Rais Biden anakabiliwa na shinikizo ndani ya chama chake cha 'Demokratik' kumtaka atowe wito wa kusitishwa mapigano.

"Kama muungaji mkono mkubwa wa kijeshi wa Israel, Marekani inawajibika kwa sehemu fulani kwa mambo yanayotokea Gaza," alisema Pramila Jaypal, mbunge Mdemokrat, alipozungumza na NBC.

Ilibainishwa kuwa Rais Biden alizungumza pia na Rais Abdel Fatah al-Sisis na kumshukuru kwa jukumu lake la kuwasilisha msaada wa dharura huko Gaza.

Pia walikubaliana kufanya kazi pamoja kuweka masharti ya kuwapo na amani ya kudumu Mashariki ya Kati pamoja na kuundwa kwa taifa la Wapalestina. **DW, VOA**

## Mfalme Charles atakiwa kuomba msamaha Kenya

**NAIROBI, Kenya**

TUME ya Haki za Kibinadamu nchini Kenya, ambayo ni shirika lisilo la kiserikali, imesema Mfalme Charles III anapaswa kuomba msamaha taifa hilo kwa unyanyasaji uliofanywa na Uingereza wakati wa ukoloni katika nchi hiyo.

Inaelezwa kuwa zaidi ya 10,000 waliuawa wakati mamlaka ya Uingereza ilipokandamiza vuguvugu la kupigania uhuru katika miaka ya 1950 - 1,000 walinyongwa baada ya kudaiwa kupatikana na makosa.

Kundi la haki za binadamu lilisema linatarajia ombi la msamaha wa umma usio na shaka kutoka kwa mfalme.



Miaka 10 iliyopita, serikali ya Uingereza ilitambua rasmi kwamba watawala wa kikoloni walifanya ukatili. Pia Uingereza ilionyesha masikitiko yake ya dhati na kukubali kulipa fidia kwa maelfu ya waveterani wa uasi huo.

Baadhi ya jamii za Wakenya, ikiwa ni pamoja na Nandi, Kipsigis na Pokot pia wanadai kuombwa msamaha na fidia ya kifedha kutoka kwa serikali ya Uingereza kwa dhuluma za kihistoria zilizofanywa dhidi yao wakati wa utawala wa kikoloni.

Baadhi ya jumuiya hizo pia zinaitaka Uingereza kurudisha mali zao za kitamaduni na ardhi za mababu zao, ambazo zilinyakuliwa na utawala wa kikoloni na bado zinashikiliwa na vyombo vya Uingereza. **BBC**




Miongoni mwa wananchi wa Kipalestina wanaoripotiwa kukwama katika hospitali ukanda wa Gaza. **PICHA: MTANDAO**

# Waliokuwa chini ya RSF wazuiliwa Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

JESHI la Sudan linasema limewazuia watoto waliokuwa wamelazimishwa kuwasaidia wapiganaji wa Kikosi cha Msaada wa Haraka RSF katika makabiliano yanayoendelea.

Kwa mujibu wa televisheni inayomilikiwa na serikali ya Sudan, watoto hao ambao idadi yao haijawekwa wazi, walikuwa wanazuiliwa katika eneo la Wadi Saidna, kaskazini mwa mji wa Khartoum.

Septemba 15, mwaka huu Jeshi la Sudan liliwasilisha watoto 30 waliokuwa wanazuiliwa kama wafungwa wa kivita kwa Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu.

Ilielezwa kuwa wapiganaji wa RSF wamekuwa wakituhumiwa mara kwa mara kwa kujihusisha na visa vya ukiukaji wa sheria za kimataifa kwa kuwasajili watoto katika mzozo unaoendelea nchini Sudan.

Mapigano yamekuwa yakiendelea kati ya wapiganaji wa RSF na jeshi mjini Khartoum, Darfur na Kordofan licha ya wito wa kusitishwa kwa vita hivyo ambavyo vimewaathiri maelfu ya watu.

Wito umeendelea kutolewa kwa kurejelewa kwa mazungumzo ya nchini Saudi Arabia yanayolenga kuafikia makubaliano ya kumaliza mapigano. **RFI**

HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS YAAPA KUIMALIZA BOTSWANA KUFUZU OLIMPIKI LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Soka ya Tanzania ya Wanawake, Twiga Stars, leo saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, itashuka kwenye Uwanja wa Taifa wa Botswana jijini Gaborone kucheza dhidi ya Botswana, katika mechi ya mkondo wa pili ya kufuzu fainali za Olimpiki zitakazofanyika mwakani nchini Ufaransa.

**Twiga itaingia uwanjani ikiwa na mtaji wa mabao 2-0 iliyoyapata nyumbani Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.**

Yalikuwa ni mabao ya Aisha Masaka na Opa Clement ambayo yamewaweka Watanzania wakiwa kwenye matumaini ya kusonga mbele kama itaweza kupata sare au kufungwa bao lisilozidi moja.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, amesema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu tayari timu zote zimeshasomana mbinu na uwezo tofauti na mwanzo ambapo hata walimu wa pande zote mbili wakiwa hawajui wapinzani wao wanacheza vipi.

"Tulikuwa na michezo miwili, wa kwanza tumecheza na kupata matokeo mazuri, na huu wa marudiano tutakuwa na kazi mbili, kushinda mchezo na kulinda matokeo tuliyoyapata Dar es Salaam ili tusonge mbele, tunaamini haiwezi kuwa mechi rahisi hata kidogo kwa sababu inawezekana walikuwa hawajui sisi tunacheza vipi na sasa wametufahamu,



wamejua ubora wetu na udhaifu na makosa yetu, hivyo wao si wajinga, ni lazima watengeneze mfumo wa kutudhibiti," alisema kocha huyo.

Aidha, alisema na yeye pia amewasoma na mkakati wake kwenye mechi ya leo ni kushambulia mwanzo mwisho.

"Na sisi pia tuna faida, tumewaona jinsi wanavyocheza, tumeona ubora na udhaifu wao, leo pamoja na kwamba tuko ugenini, lakini tutakachofanya kwanza ni kuwashambulia, kwa sababu tunaamini njia bora ya kujilinda ni kushambulia, lakini kumiliki mpira kwa muda mrefu kwa sababu tukiwa na mpira hawawezi kutufunga, watatufunga tu pindi na wao watakapokuwa na mpira, kwa hiyo hatukuja hapa kuuweka mpira nyuma. Tumekuja kucheza, kushambulia na kumiliki mpira kwa muda mrefu wa mchezo na kwa uwezo wa wachezaji wetu hilo litafanikiwa," alitamba Shime.



Baadhi ya wanamichezo wa jogging wakizunguka mitaa ya Tandale, Dar es Salaam juzi kwa ajili ya kampeni ya kupinga rushwa ya ngono. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Jogging kupiga vita rushwa ya ngono*

**Na Sabato Kasika**

MAKUNDI ya jogging yametakiwa kushiriki katika vita ya kupinga rushwa ya ngono, ili kuwalinda mabinti dhidi ya rushwa hiyo waweze kutimiza ndoto zao katika elimu.

Hayo yalisemwa na Diwani ya Kata ya Tandale jijini Dar es Salaam juzi, Abdallah Said, wakati akizungumza na makundi hayo baada ya kumaliza mbio za jogging.

Mbio hizo ziliandaliwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) kwa kushirikiana na madereva bodaboda, bajaj na daladala wa Kata ya Makumbusho.

Akizungumza kwa niaba ya diwani huyo, Katibu wake, Muhidin Mtengeleka, alisema makundi ya jogging yana nafasi kubwa ya kuhamasisha vita dhidi hiyo tabia hiyo, kwa kuwa yanahusisha vijana wa kike na wa kiume.

"Ninawashukuru WAJIKI kwa kuleta na makundi ya jogging kutoka Kata ya Makumbusho kuja huku kwetu kuhamasisha vita hii, nami ninawaomba muwe mstari mbele kufanya kazi hii, kwani rushwa ya ngono imekithiri maeneo mengi," alisema Mtengeleka.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema walipeleka Kampeni ya Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono, Tandale kwa kuwa eneo hilo ni miongoni mwa yale yaliyoshamiri vitendo hivyo.

"Tumeamua kuja huku kwa kushirikiana na makundi ya jogging kwani nayo yana ushawishi wa kusaidia katika vita hii ya kuwanusuru watoto wa kike na hata wa kiume dhidi ya ulawiti," alisema Janeth.

Alifafanua kuwa makundi ya michezo mbalimbali yakiwamo ya jogging yanakutanisha vijana wengi, na kwamba yakitumika vema yanaweza kusaidia harakati za kupinga rushwa ya ngono nchini.

"Tutaendelea kupanua kampeni hii hadi kwa wachezaji wa mpira wa miguu ili nao watusaidie katika vita hii, kila wafadhili wetu Women Fund Tanzania (WFT) watakapotuwezesha," alisema.

## KMKM SC yaanika siri kuichapa KVZ SC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kuwachakaza Maafande wenzao wa KVZ SC kwa mabao 2-0 katika mchezo wa kukamilisha mzunguko wa nane wa Ligi Kuu Zanzibar juzi, Kocha Msaidizi wa KMKM SC, Ame Msimu, amesema malengo yao yametimia ya kuhakikisha kwenye mchezo huo wanapata alama tatu huku akiweka wazi kuwa kupambana kwa wachezaji wake ndio silaha ya ushindi huo.

Katika mchezo huo, mabao ya KMKM yalifungwa na Yahya Ramadhani dakika ya 83 na Ibrahim Is-haka dakika ya 88, hivyo kuifanya KVZ kupoteza mechi ya pili tangu kuanza kwa msimu huu wa 2023/24, wakati huu ikiwa imeshashuka dimbani mara nane.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kocha Msaidizi wa KMKM, Msimu alisema malengo yao yametimia ya kuhakikisha mchezo huo wanapata alama tatu na kuendelea kujiweka katika mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

Alisema licha ya kupata ushindi katika dakika za mwishoni, lakini mchezo ulikuwa mgumu zaidi hasa pale mchezaji wao mmoja alipotolewa kwa kadi nyekundu katika kipindi cha kwanza na kucheza wakiwa pungufu.

Msimu alisema wachezaji walijituma zaidi na kufanikiwa kupata alama tatu katika mchezo ambao ni muhimu kulingana na msimamo wa ligi ulivyo.

"Tumefanikiwa kupata alama tatu ambazo ndizo zilikuwa malengo yetu makubwa hasa kushinda katika mchezo huu, pongezi kwa wachezaji ambao walijituma sana hasa wakiwa pungufu uwanjani, hili limeisha hivyo tunajipanga na mchezo ujao wa mzunguko wa tisa," alisema Msimu.

Kocha Mkuu wa KVZ, Ali Mohmed Ameir, alisema kupoteza mchezo huo kumetokana na kukosa umakini kwa safu ya ulinzi hasa upande wa kushoto ambapo mashuti yote ya mabao yalitokea.

Alisema kipindi cha kwanza kilikuwa kigumu licha ya timu yake kufanikiwa kumiliki mpira, cha pili wachezaji walikuwa wakipoteza mipira ovyo pamoja na kukosa nafasi nyingi za wazi.

Kwa Matokeo hayo Maafande wa JKU wameendelea kubaki kileleni kwa alama zao 17, nafasi ya pili inashikiliwa na KMKM ikiwa na pointi 16 sawa na KVZ ambao wenye wapo nafasi ya tatu kutokana na kuzidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### LUKAKU KUBADILISHWA

AS Roma inafikiria kumkabidhi mshambuliaji wa England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 26, kwa klabu yake ya zamani ya Chelsea katika mkataba wa kubadilishana mshambuliaji wa 'The Blues' na Ubelgiji Romelu Lukaku mwenye miaka 30, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu hiyo ya Italia. ***(Mirror)***

#### MBAPPE, HAALAND WAWINDWA

REAL Madrid inapanga kuwasajili mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, kutoka Paris St-Germain na straika wa Manchester City na Norway, Erling Haaland, 23. ***(El Chiringuito, via 90 min)***

#### GUEHI SASA AGOMBEWA

KLABU za Arsenal, Manchester United na Manchester City zote zina nia ya kumsajili beki wa Crystal Palace na England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23. ***(Goal)***

#### CHELSEA KUSAKA BEKI

CHELSEA itamsaka beki na mshambuliaji katika dirisha la usajili la Januari. ***(Fabrizio Romano)***

#### RAMSDALE KUPIGWA BEI

ARSENAL iko tayari kumuuza kipa wa England, Aaron Ramsdale, msimu ujao baada ya kubadili nia yao kuhusu mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

#### TRINDADE NA LIVER, ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Fluminense, Mbrazil Andre Trindade mwenye umri wa miaka 22, amesema alikataa kuhama msimu wa majira ya joto, huku Liverpool na Arsenal zikimwania, akiwa na nia ya kuisaidia timu yake kushinda Copa Libertadores. ***(90 min)***

#### MUSIALA ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Bayern Munich Mjerumani Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20, ambaye hajaridhishwa na muda anaopewa kucheza klabuni kwake. ***(Mirror)***

#### LUIZ MKATABA MPYA

ASTON Villa inajiandaa kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo wa Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, ambaye Arsenal wanamhusudu. ***(Football Insider)***

#### TADIBO AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mchezaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23 na beki wa Nice, Jean-Clair Todibo. ***(Fabrizio Romano)***

#### TONEY KWA ARSENAL, SPURS

ARSENAL na Tottenham zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, lakini hawako tayari kulipa dau la pauni milioni 61. ***(Fichajes)***

#### LINGARD ATAFUTA TIMU

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard, anatafuta klabu mpya kwa sababu Al-Ettifaq hawana nafasi katika kikosi chao. ***(Star)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: HIKI NI KIPIGO KIBAYA SANA KWANGU

**Ni baada ya Man City kuipelekea moto United wa mabao 3-0 pale Old Trafford...**

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesema kichapo kizito cha Manchester United katika mchezo wa dabi kutoka kwa Manchester City kilikuwa moja ya siku mbaya zaidi tangu awe kocha hapo Old Trafford.

**City walipata ushindi wa 3-0 Jumapili kwa mabao mawili kutoka kwa Erling Haaland, ikijumuisha penalti ya kipindi cha kwanza, na lingine kutoka kwa Phil Foden.**

Ten Hag amepata matokeo mabaya kama kocha wa United, lakini aliulizwa kama kipigo hicho kutoka kikosi cha Pep Guardiola kiliifanya kuwa moja ya siku mbaya zaidi katika kazi hiyo, alijibu: "Ndiyo."

Aliongeza: "Ni kweli, inasikitisha, lakini mwaka jana tulikuwa na mambo muhimu mengi. Unapopoteza dabi kwa jinsi tunavyopoteza, hiyo inakatisha tamaa.

"Kipindi cha kwanza tulikuwa na mpango mzuri sana wa mchezo na utekelezaji ulikuwa mzuri sana. Lakini, katika kipindi cha pili mambo yalibadilika haraka sana. Kuanzia hapo ulikuwa mchezo mgumu."

United sasa wamepoteza mechi tano kati ya 10 za kwanza za ligi kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1986 na wanashika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, wakiwa na pointi 11 nyuma ya vinara Tottenham Hotspur.

Sasa ni vipigo saba kutoka mechi 14 za mashindano yote msimu huu, lakini Ten Hag alisema ana imani timu yake inapiga hatua.

"Mechi tatu kabla ya sisi kushinda na roho ni nzuri sana," Ten Hag alisema.

"Nafikiri tupo njiani, mwanzo ulikuwa mgumu, lakini sasa tupo njiani, walio majeruhi watakaporejea tutakuwa tunazidi kuimarika, inabidi tuwe wavumilivu, lakini nafurahi baadhi ya walio majeruhi wanarudi na baadaye upande wetu utakuwa na nguvu zaidi."

Baadaye, Ten Hag alisema alisimama na uamuzi wake wa kuwaacha Raphael Varane na Sergio Reguilon kwenye benchi akipendelea Jonny Evans na Victor Lindelof huku pia akitetea uamuzi wake wa kuchukua nafasi ya mshambuliaji Rasmus Højlund katikati ya kipindi cha pili baada ya mabadiliko kupokelewa kwa sauti kubwa.

"Lazima nimlinde Rasmus Højlund na lazima niilinde timu," Ten Hag aliongeza.

# GUNDOGAN ATAKA ZAIDI BARCELONA




**BARCELONA,** Hispania

ILKAY Gundogan amesema Barcelona lazima ioneshe hisia na hasira zaidi ikiwa inataka kushindana katika michezo mikubwa zaidi baada ya kupoteza El Clasico Jumamosi kwa kufungwa mabao 2-1 na Real Madrid kwenye Uwanja wa Olympic.

Barca walichukua uongozi katika kipindi cha kwanza kupitia kwa Gundogan, lakini mabao mawili ya Jude Bellingham yaliisaidia Madrid kurejea kileleni mwa LaLiga.

Gundogan alisema jinsi Barca walivyochukulia kichapo hicho iliangazia matatizo watakayokumbana nayo ikiwa wanataka kuwania taji hilo msimu huu.

"Lazima niwe mkweli, si kama ninavyotamani kwa sababu sitaki kusema kitu kibaya, lakini nilikuwa kwenye chumba cha kubadilishia nguo na bila shaka watu wamekata tamaa," alisema kiungo huyo wa kati wa Ujerumani akiiambia LaLiga TV.

"Lakini haswa baada ya mchezo mkubwa kama huu na matokeo yanayoumiza, natamani kufadhaika zaidi, hasira zaidi na tamaa zaidi. Hili ni shida kidogo.

"Lazima kuwe na hisia zaidi, haswa unapopoteza na unapojua unaweza kufanya vizuri zaidi, fanya vizuri zaidi katika hali fulani.

"Inahamia uwanjani mwisho wa siku. Tunahitaji kupiga hatua kubwa katika hilo kwa sababu vinginevyo Real Madrid au hata Girona watakimbia. Sikuja hapa kupoteza aina hii ya mchezo.

## Emery aiweka Villa nne bora

**LONDON,** England

UNAI Emery ana uhakika Aston Villa inaweza kuwa mshindani kwenye nne bora msimu huu baada ya kuendeleza kiwango chao cha ajabu kwa ushindi mnono dhidi ya Luton, Jumapili.

Villa waliendelea na kasi ya nne bora kwenye Ligi Kuu England wakati wa ushindi mkubwa wa mabao 3-1 katika Uwanja wa Villa Park ambao ulishuhudia John McGinn na Moussa Diaby wakifunga pamoja na Tom Lokyer aliyejifunga.

Ulikuwa ushindi wa 12 mfululizo kwa Villa nyumbani na ushindi wa tano, huku matumaini ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya yakiwa juu.


Kuhusu nafasi za timu yake, Emery alisema: "Lazima uwe mhitaji sana na uzingatie kila mechi.


"Tunashinda mechi kwa sababu tunazingatia sana, tunahitaji sana mfumo wetu wa ulinzi, tunajaribu kujenga timu yenye kujituma kwa hali ya juu.

"Tuko kati ya timu nyingine saba, zinaonesha nguvu zao mara kwa mara.

"Lakini ikiwa tunafanya kazi hivyo na kufanya mchakato huu, tukidai, tukiwa na nguvu, bila shaka tunaweza kuendelea na bado kuweka wakati tulionao kwenye meza.

"Nataka kukabiliana na kila mechi nikiwa na umakini, kujiandaa ipasavyo na kuhitaji.





## Klopp aelezea ugumu mechi dhidi ya Forest

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Jurgen Klopp, alisema maandalizi ya ushindi wa mabao 3-0 nyumbani dhidi ya Nottingham Forest Jumapili yalikuwa "magumu zaidi ambayo nimewahi kuwa nayo maishani".

Mshambuliaji wa 'Wekundu' hao, Luis Diaz hakushiriki katika mechi ya Ligi Kuu England kwenye Uwanja wa Anfield baada ya ripoti kwamba wazazi wake walitekwa nyara nchini Colombia na Klopp alisema mchezaji huyo alirejea nyumbani kuwa na wanafamilia.

Liverpool ilithibitisha "hali inayoendelea inayohusisha familia ya Luis Diaz" mapema Jumapili na Rais wa Colombia alisema mama wa Diaz "ameokolewa", lakini baba yake bado.

Klopp alisema: "Maandalizi ya mchezo yalikuwa magumu zaidi ambayo nimewahi kuwa nayo katika maisha yangu. Sikutarajia hilo, sikuwa tayari kwa hilo.

"Sikutaka kuufanya mchezo kuwa mkubwa zaidi ya ulivyokuwa, lakini kwa hakika, tulijaribu kumsaidia Luis kwa pambano tulilopiga kwa sababu ni wazi tunataka kusaidia na hatuwezi kusaidia.

"Kwa hiyo kitu pekee tunachoweza kufanya ni kumpigania na ndivyo vijana walivyofanya."

Liverpool walipata ushindi wao wa tano mfululizo nyumbani wa Ligi Kuu na kusonga mbele kwa pointi tatu nyuma ya vinara Tottenham, Arsenal na Manchester City.

Lakini Klopp alisema: "Unawezaje kuufanya mchezo wa soka kuwa muhimu sana katika siku kama hii? Ni ngumu sana. Sijawahi kuhangaika na hilo maishani mwangu.

"Tulisikia usiku kuhusu jambo hilo. Tulizungumza na Luis, alitaka kurudi nyumbani... kisha tukapata habari ya mama yake, ambayo ni ya ajabu, na tangu wakati huo hakuna kitu kabisa.

"Kwa kweli sisi ni watu wa kwanza kuhusika na tunajaribu kuwa na ufahamu wa kila kitu kadri tuwezavyo, lakini hatutaki kuwasumbua kwa njia yoyote watu muhimu huko, tunataka tu kuunga mkono, ndivyo hivyo."

Liverpool walisema katika taarifa yao kuwa wanamuunga mkono mchezaji huyo. Ilisomeka: "Klabu ya Soka ya Liverpool inaweza kuthibitisha kuwa inafahamu kuhusu hali inayoendelea inayohusisha familia ya Luis Diaz huko Colombia.

## Yanga yamtaja

INATOKA UKURASA 24

Simba hajawahi kufungwa dhidi ya Yanga, bali hajapoteza mechi yoyote akicheza na timu hiyo tangu akiwa kwenye klabu zingine za Ukanda wa Cecafa ikiwamo wakati akiinoa Vipers ya Uganda na klabu zingine za nchini Rwanda.

Alisema wachezaji wameahidiwa zaidi ya Sh. milioni 100 kama watabuka na ushindi, lakini wao kama viongozi wanazitaka pointi tatu ambazo kama zikipatikana watakuwa pia wamevunja mwiko wa kutopata ushindi dhidi ya Robertinho.

Kigogo huyo alisema baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Singida Fountain Gate FC na kuchomoza na ushindi wa mabao 2-0, walikutana na wachezaji na benchi la ufundi kuzungumzia maandalizi ya mchezo wao ujao dhidi ya Simba.

"Hii ni dabi, mechi kubwa na hata maandalizi yake yanakuwa makubwa, ukizingatia tulipoteza alama mbele ya Simba safari hii hatutaki kuona hilo linajirudia, tunajipanga vizuri zaidi," alisema mtoa habari huyo.

Ikumbukwe tangu Robertinho amekabidhiwa mikoba ya kukinoa kikosi cha Simba hajawahi kupoteza mbele ya Yanga, mechi ya kwanza walitoka sare, mzunguko wa pili walikubali kichapo na mara ya tatu Yanga walifungwa kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya Ngao ya Jamii iliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, baada ya juzi kuishuhudia mechi ya Simba dhidi ya Ihefu FC, jana ameliambia Nipashe kuwa anajivunia timu yake kwa kazi kubwa inayofanyika na amerudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi baadhi ya vitu kabla ya kukutana na watani wao hao wa jadi.

Alisema kazi kubwa ni kuwa makini kwa baadhi ya nyota wake akiwamo Stephane Aziz Ki, Pacome Zouzoua na Maxi Nzengeli kuhakikisha wanakuwa makini kutumia vema nafasi wanazopata ili kufunga mabao.

"Mechi iliyopita dhidi ya Singida tumeshinda, lakini tumepoteza nafasi nyingi, hili ni tatizo na tunalifanyia kazi eneo la mbele, ili kutumia vema nafasi tunazotengeneza," alisema Gamondi.

# KABURU, DEWJI WAFUNGUKA KUTEULIWA KUISHAURI SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, ameteua wanachama 21 wa klabu hiyo kuwa wajumbe wa Bodi ya Baraza la Ushauri wa klabu, ambapo baadhi walioteuliwa ni watu maarufu waliowahi kuwa viongozi wa nyadhifa mbalimbali, akiwamo Ismail Aden Rage, Geofrey Nyange 'Kaburu', Hassan Dalali, Azim Dewji, Kassim Dewji, Swedi Nkwabi, Evance Aveva, Mwina Kaduguda na wengineo.

**Katika uteuzi huo alioutangaza jana mchana, Mo amesema mojawapo ya majukumu yake kama Rais wa Heshima ni kuhakikisha uongozi na utawala bora unazidi kuboreka kila wakati ili kuzidi kusukuma gurudumu la maendeleo ya klabu hiyo.**

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tangu tuanze safari ya mabadilikilko klabu yetu imepiga hatua kubwa sana katika nyanja mbalimbali.

Pamoja na maendeleo ambayo klabu yetu imepiga katika kipindi hiki cha miaka mitano, lakini malengo yetu bado hatujayafikia.

Hivyo basi, baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi na Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, nimewateua wanachama hawa kuwa Wajumbe wa Baraza la Ushauri (Advisory Board) la Klabu ya Simba," alisema Mwekezaji huyo.

Jaji Thomas Mihayo ndiye aliyechaguliwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, huku wajumbe wake wengi wakiwa waliowahi kushika nyadhifa kwenye klabu hiyo kama Uenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Rais wa Klabu, Katibu Mkuu, Mfadhili Mkuu na nyinginezo.

Mbali na hao, wengine walioteuliwa ni Faroukh Baghoza, Musleh Al-Ruweh, Mohamed Nassor, Mulamu Ng'ambi, Octavian Mshiu, Profesa Mohamed Janabi, Hassan Kipusi, Gerald Yambi, Moses Kaluwa, Crescentius Magori, na Idd Kajuna.

WEWE!...




Winga wa Manchester City, Jeremy Doku (kulia), akimuonya mshambuliaji wa Manchester United, Antony, kwa kumchezea rafu mbaya katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi kwenye Uwanja wa Old Trafford na United kuchezea kichapo cha mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## Mbeya City hoi kwa Stand Utd Ligi ya Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City ambayo inahangaika kutaka kurejea Ligi Kuu msimu ujao baada ya kushuka msimu uliomalizika, juzi ilijikuta ikiangukia pua kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Stand United katika mechi ya raundi ya nane ya Ligi ya Championship iliyopigwa Uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga.

Bao pekee kwenye mchezo huo lilifungwa na Emmanuel Mtambuka dakika ya 30 ya mchezo, likiipeleka Stand United hadi nafasi ya tisa ya msimamo ikiwa na pointi 11, Mbeya City nayo ikibaki nafasi ya nane kwa pointi kama hizo.

Kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, wenyeji Cosmopolitan walipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania.

Matokeo hayo yanaifanya timu hiyo ambayo ni Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1967, kufikisha pointi nane, ikiwa nafasi ya 13 ya msimamo wa ligi hiyo, huku maafande hao ambao nao walishuka msimu uliopita wakibakia na pointi 13, katika nafasi ya sita kwenye ligi hiyo.

Maafande wa Transit Camp, wakiwa Uwanja wa Jamhuri Morogoro, walilazimishwa suluhu dhidi ya Mbuni FC.

Ni matokeo yaliyoisogeza Mbuni kwenye nafasi ya tano ya msimamo ikiwa na pointi 14, Transit Camp ikiwa chini kwenye nafasi ya 15 na pointi zake tano kwenye ligi hiyo ambayo inaongozwa na KenGold yenye pointi 19, na Ruvu Shooting ikikamata mkia na pointi yake moja mpaka sasa.

## Phiri bado yupo sana Simba

INATOKA UKURASA 24

hatoenda popote, badala yake atabaki kuwa mchezaji wa timu hiyo na suala la kutopata nafasi linabaki kuwa jukumu la Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira.

Ahmed alisema Phiri bado ni mali yao na hawafikirii kuachana na nyota huyo ambaye kila anapopata nafasi hufanya vizuri.

Aliongeza kuwa nyota huyo atakuwa sehemu ya kikosi kinachoingia kambini leo kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga, utakaochezwa Jumapili wiki hii katika



Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Ni kweli kuna taarifa tunaziona juu ya Phiri, ukweli ni kuwa mchezaji huyo bado ataendelea kubaki ndani ya klabu hii, inapofikia kipindi cha usajili utaona Yanga inatajwa kuchukuwa baadhi ya nyota wetu.

"Suala la kupata nafasi ya kucheza liko chini ya kocha Robertinho, ukizingatia kuna mechi nyingi na tunaimani Phiri au mchezaji yeyote ndani ya Simba watapata nafasi ya kucheza," alisema Ahmed.

Katika mechi tatu ambazo Phiri amepata nafasi kipindi cha pili akitokea benchi, zote amefunga bao ikiwamo ya Jumamosi iliyopita ambayo Simba ilishinda mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Michezo

Jumanne Oktoba 31, 2023

Nipashe



'Hiki ni kipigo kibaya kwangu' UKURASA 21

# Yanga yamtaja Robertinho dabi, Simba na mkakati mzito

●●● Yataka kuvunja utawala wake, kuziona buku 10, Wekundu wasema utakuwa ushindi wa jasho...

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mechi ya 'Dabi' ya Kariakoo Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, wenyeji wa mchezo huo wa Ligi Kuu Bara, Simba, wametangaza mkakati wao kabambe wa kuzitaka pointi tatu huku Yanga wakieleza mbali na alama tatu wanataka pia kuvunja utawala wa Kocha Robertinho Oliveira wa kuwaadhibu kila wanapokutana na timu anayoifundisha.

BALEKE

**Miamba hiyo inakutana Jumapili huku ikiwa na pointi sawa (18), Yanga ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kutokana na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa, lakini Simba inafaida kutokana na kuwa na mchezo mmoja mkononi.**

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema mipango yao ni kutafuta alama 15 za awamu ya pili katika michezo mitano wakianza na pointi tatu dhidi ya Yanga.

"Msimu huu tumegawa mechi zetu katika awamu sita kwenye michezo yetu ya Ligi Kuu, mechi tano kila awamu, tumemaliza awamu ya kwanza kuvuna alama 15, sasa tunaenda hatua ya pili ambayo mechi ya kwanza na Ihefu FC tumemaliza.

"Kazi kubwa ipo mechi nne zilizosalia ikiwamo dhidi ya Yanga, tunahitaji kupata alama tatu muhimu ili kujiweka katika ramani ya dhamira yetu ya msimu huu kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema.

Alisisitiza kuwa wameingia kambini mapema jambo ambalo si kawaida yao, kwa mechi za ndani ambazo wamekuwa wakiingia siku tatu kabla, lakini safari hii wameingia siku sita kabla ya kukutana na Yanga.

"Simba tunahitaji hii mechi na kupambana kuendeleza ubabe wetu kwa muda wote, lazima tuhakikishe tunapata ushindi ili kufiki dhamira yetu ya kutwaa ubingwa," alisema Meneja huyo.

Aliongeza kuwa wamedhamiria kutwaa ubingwa mapema na ili kufika huko lazima wamfunge Yanga katika mchezo wao wa Jumapili na kurejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

"Azam FC tayari ameshajitoa katika mbio za ubingwa na kazi iliyosalia ni kumfunga Yanga, mechi ya Jumapili tumedhamiria kuendeleza ubabe wetu kwa watani wetu, baada ya mchezo wa Ihefu FC tukaanza maandalizi ya mechi dhidi ya Yanga. Simba tumewekeza nguvu nyingi sana kwa sababu ukipoteza au kushinda basi tutakumbuka milele.

"Hatuwezi kukataa kuwa Yanga wamekuwa na kikosi bora, wachezaji wanapambana, tumefuatilia mechi zao na tunaenda kukutana na mpinzani ambaye yuko fiti, licha ya ubora wetu lakini tunatakiwa kutafuta ushindi kwa jasho ili kufikia malengo yetu ya kusaka alama tatu katika mechi tano za hatua ya pili," alisema.

Alitaja viingilio vya mchezo huo kuwa viti vya machungwa ni Sh. 10,000, VIP C Sh. 20,000, VIP B Sh. 30,000 na VIP A Sh. 40,000 huku Platinum ikiwa ni Sh. 150,000.

Kwa upande wa Yanga, kigogo mmoja, ambaye yupo karibu na Nipashe, ameliambia kuwa pamoja ya kwamba ni kawaida zinapokuja mechi kama hizi kuweka bonasi, lakini hii imekwenda mbali zaidi kwani wanataka kulipa kisasi cha kufungwa kwa penalti kwenye mechi ya Ngao ya Jamii jijini Tanga, lakini kupata ushindi dhidi ya Kocha Robertinho, ambaye si tangu tu atue

INAENDELEA UKURASA 23



## Phiri bado yupo sana Simba

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuanza kuhusishwa na kutimkia Yanga kuelekea dirisha dogo litakalofunguliwa Desemba mwaka huu, uongozi wa Klabu ya Simba umeibuka na kuwatoa hofu wanachama na mashabiki wao kwa kueleza kuwa Moses Phiri, haendi popote.

Klabu hiyo imesema hivyo, baada ya tetesi kuwa nyota huyo anahitaji kuondoka ndani ya klabu hiyo huku akitajwa kutua kwa wapinzani wao, Yanga dirisha hilo litakapofunguliwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema Phiri

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >